**JAMHURI YA KENYA**
**WIZARA YA ELIMU**

# MTAALA WA SHULE YA MSINGI

# KISWAHILI

# GREDI YA 4

# KWA WANAFUNZI WALIO NA CHANGAMOTO ZA KUONA

**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**
**JAMII ADILIFU NA YENYE UJUZI**

Chapisho la Kwanza 2017

Chapisho la Pili 2022

Chapisho la Tatu 2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

**ISBN: 978-9914-43-069-1**

Kimechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

## UTANGULIZI

Serikali ya Kenya inajitolea kuhakikisha kuwa malengo ya sera kuhusu elimu, mafunzo, na utafiti yanakidhi matarajio ya Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya Kenya 2030, Sera ya Mtaala wa Kitaifa ya 2019, Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs), na mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo Kenya imesaini. Kuelekea kufikia lengo la Elimu ya Msingi, Wizara ya Elimu (MoE) imetekeleza kwa mafanikio na hatua kwa hatua utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi (CBC) katika ngazi ya awali, msingi, na Shule za Upili za daraja la chini.

Utekelezaji wa Mtaala wa Kitaalamu unajumuisha ufuatiliaji na tathmini ili kubaini mafanikio yake. Baada ya mzunguko wa miaka mitano wa utekelezaji, tathmini ya jumla ya mzunguko wa elimu ya msingi ilifanywa ili kubaini kufikia malengo ya matokeo ya kujifunza kama ilivyotarajiwa katika Mfumo wa Mtaala wa Elimu ya Msingi.

Serikali ya Kenya iliunda Jopo Kazi la Rais kuhusu Mageuzi ya Elimu'Presidential working party on Education Reforms' (PWPER) mwaka 2022 kushughulikia masuala muhimu yanayoathiri sekta ya elimu. PWPER ilifanya mapendekezo mapendekezo mbalimbali yaliyochangia marekebisho ya mtaala.

Mapendekezo ya PWPER, ripoti za ufuatiliaji, tathmini ya jumla, maoni kutoka kwa watekelezaji wa mtaala, na wadau wengine yalisababisha hatua ya kufanya marekebisho katika mtaala pamoja na kuchunguza upya masomo yaliyopendekezwa.

Mtaala wa Gredi ya **4** kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona uliofanyiwa marekebisho, umejengwa kutokana na umilisi uliokuzwa katika gredi ya **tatu**. Umuhimu katika gredi hii ni maendeleo ya usomaji wa msingi, hesabu, na stadi za mwingiliano na mazingira.

Mitaala hii inawakilisha Malengo ya Kitaifa ya Elimu, kauli kiini, matokeo yanayotarajiwa kwa ujumla na kwa kila somo pamoja na Mada na Mada Ndogo. Mitaala hiyo pia inajuimuisha Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa, Swali Dadisi Lililopendekezwa, Umilisi wa kimsingi unaokuzwa, masuala mtambuko(PCI's), maadili, vigezo na viwango vya kuzingatia katika kutathmini.

Ni matumaini yangu kuwa mashirika yote ya serikali na wadau wengine katika Elimu watatumia miundo hii ili kuwezesha ufanisi na utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi katika kiwango hiki.

**HON. EZEKIEL OMBAKI MACHOGU, CBS**
**WAZIRI WA ELIMU**
**WIZARA YA ELIMU**

**DIBAJI**

Wizara ya Elimu (MoE) ilianza kutekeleza Mtaala wa Kiumilisi (CBC) mwaka 2019 nchini kote. Gredi ya Kwanza ndiyo ya kwanza katika ngazi ya Elimu ya Msingi nayo Gredi ya Sita ni ya mwisho katika ngazi hiyo katika mfumo uliofanyiwa marekebisho wa elimu.

Mtaala uliofanyiwa marekebisho wa Gredi ya 4 unaendeleza utekelezaji wa Mtaala wa Umilisi kutoka Gredi ya 3 katika ngazi ya Msingi. Mtaala huu unatoa fursa kwa wanafunzi kuzingatia wanachokipenda ili kuunda msingi wa elimu na mafunzo zaidi na/au kupata stadi za ajira. Kiwango hiki cha elimu ni muhimu sana katika kuchangia kufikia ruwaza na mwito wa marekebisho yanayoendelea ya kimtaala kama ilivyoelekezwa katika Mswada Elekezi Nambari 1 wa mwaka 2019 kuhusu Kuelekea kuafikia elimu na mafunzo yenye ubora, faafu na jumuishi kwa maendeleo endelevu nchini Kenya ''*Towards Realizing Quality, Relevant and Inclusive Education and Training for Sustainable Development'*. Mswada Elekezi huo unaeleza kuhusu kuvuka kutoka mtaala wa Kimafunzo na kuzingatia kukuza vipawa vya kila mwanafunzi.
Hivyo basi, mtaala wa Gredi ya 4 kwa wanafunzi walio na *changamoto za kuona* inalenga kuimarisha ukuzaji wa Umilisi wa Kimsingi katika mtaala huu, yaani: mawasiliano na ushirikiano, uwazaji kina na utatuzi wa matatizo, ubunifu, uraia, ujuzi wa kidijitali, hamu ya kuendelea kujifunza na kujiamini.
Mitaala inapendekeza shughuli shirikishi za ujifunzaji unaolingana na Mada Ndogo mbalimbali na vipengele vingine vya mtaala wa umilisi (CBC). Pia inapendeza baadhi ya nyenzo za kufundishia na mbinu za kutathmini mbalimbali. Inatarajiwa kwamba mitaala hii itaongoza walimu kufanikisha wanafunzi kufikia matokeo maalum yanayotarajiwa ya kujifunza katika gredi ya 4 na kuwaandaa kwa mpito laini kwa Gredi ya 5. Zaidi ya hayo, ni matarajio yangu kuwa mwalimu atatumia mitaala iliyobadilishwa kufanya ujifunzaji uwe wa kuvutia unaochangamsha na wa kufurahiwa.

**DR. BELIO R. KIPSANG, CBS**
**KATIBU MKUU**
**IDARA YA SERIKALI YA ELIMU YA AWALI NA ELIMU YA MSINGI WIZARA**

**SHUKRANI**

Sheria Nambari 4 ya 2013 (Toleo jipya 2019) ya Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya (KICD) inaipa uwezo Taasisi kukuza na kufanyia marekebisho *(SNE adapt)* na vifaa vya msaada kwa mtaala kwa elimu ya msingi na ya vyuo vya Elimu na Mafunzo ya juu vilivyo chini ya vyuo vikuu. Mchakato wa ukuzaji mtaala wa kiwango chochote huhusisha utafiti, ulinganishi wa kimataifa, na uhusishaji mkubwa wa wadau. Kupitia kwa mchakato huu wa utaratibu na wa mashauriano, KICD ilizua wazo la Mtaala wa Kiumilisi (CBC) kama ilivyoelezwa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (BECF) 2017 ambao unaitikia mahitaji ya karne ya 21 na matamanio yanayoelezwa katika Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya 2030, Itifaki ya Jumuia ya Afrika Mashariki na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. (SGDs).

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya (KICD) hufadhiliwa na Serikali ya Kenya ili kutekeleza majukumu na mipangilio ya serikali na sekta ya elimu. Pia, Taasisi hupata msaada kutoka kwa mashirika mengine ya kimaendeleo yanayoangazia miradi teule.

Mtaala uliyorekebishwa Gredi ya 4 kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona ilipangwa na kubadilishwa kwa msaada wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Usawa wa Elimu ya Msingi ya Kenya katika Programu ya Kujifunza ‘Kenya Primary Education Equity in Learning Programme’ (KPEELP): mradi ulioratibiwa na MoE. Kwa hiyo, Taasisi inashukuru sana kwa msaada wa Serikali ya Kenya, kupitia MoE, na washirika wa maendeleo kwa msaada wa sera, rasilimali, na msaada wa logistiki. Kwa namna ya pekee, shukrani maalum kwa Waziri wa Elimu-MoE na Katibu Mkuu wa Idara ya Elimu ya Msingi.

Ningependa kuwashukuru wakuza mitaala wa KICD na wafanyakazi wengine, walimu wote na wanaelimu wengine walioshiriki kama wanajopo katika ukuzaji wa mitaala. Nashukuru pia mashirika mengine yanayoshirikiana na serikali (SAGAs) na wawakilishi wa wadau mbalimbali kwa majukumu mbalimbali waliyotekeleza katika ukuzaji na ubalishaji wa Mitaala ya Gredi ya 4-6 kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona. Kuhusiana na hili, ningependa kushukuru Katibu wa Tume ya Kuwaajiri Walimu (TSC) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Kitaifa la Mitihani (KNEC) kwa msaada wao katika mchakato wa kukuza na kubadilisha mitaala hii. Mwisho, ninawashukuru sana mwenyekiti wa baraza la KICD na wanachama wengine wa Baraza kwa mwongozo thabiti katika mchakato huu.

Nawahakikishia watekelezaji wa mtaala, wazazi na washikadau wengine kuwa mitaala hii itaelekeza ipasavyo utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi katika Gredi ya **4** na maandalizi ya wanafunzi walio na changamoto za kuona kwa mpito wa Gredi ya **5**.

**PROF. CHARLES O. ONG’ONDO,**
**MBS MKURUGENZI/OFISA MTENDAJI MKUU,**
**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**

## YALIYOMO

UTANGULIZI ........ viii

DIBAJI ........ ix

SHUKRANI ........ x

YALIYOMO ........ xi

MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA ........ xiii

MGAO WA VIPINDI KATIKA SHULE YA MSINGI DARAJA YA JUU ........ xv

MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA ELIMU YA MSINGI ........ xvi

KAULI KIINI ........ xvi

MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI ........ xvii

MADA ........ xvii

1.0 NYUMBANI ........ 1

2.0 NIDHAMU MEZANI ........ 16

3.0 MAVAZI ........ 27

4.0 DIRA ........ 42

5.0 USHAURI-NASAHA ........ 53

6.0 BENDERA YA TAIFA ........ 62

7.0 MATUNDA NA MIMEA ........ 71

9.0 AFYA BORA ........ 91

10.0 KUKABILIANA NA UHALIFU ........ 99

11.0 MAPATO ........ 109

MWONGOZO WA VIWANGO NA VIGEZO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA ........ 123
MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ........ 123
MADA: SARUFI ........ 126

**MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA**

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

1. **Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa**
   Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kuondoa mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana. Mielekeo hii itawawezesha wanajamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia ukuaji wa taifa.

2. **Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**
   Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa taifa la Kenya kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.

   a) **Mahitaji ya kijamii**
   Elimu nchini Kenya lazima iwatayarishe vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mageuzi taratibu ya kijamii kutokana na maendeleo ya haraka ya usasa. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kujirekekebisha kutokana na mabadiliko haya.

   b) **Mahitaji ya kiuchumi**
   Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na sifa za kibinafsi zinazohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika humu nchini.

   c) **Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**
   Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda. Kenya inatambua mabadiliko ya haraka ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunaweza kuwa sehemu ya maendeleo haya ikiwa mfumo wetu wa elimu utalenga kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko ya yanayoendelea ulimwenguni.

3. **Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**
   Elimu inapaswa kuwezesha kutambua, kukuza na kuimarisha vipawa vya kila mmoja ili kuweza kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**
   Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**
   Usawa wa kijamii kwa mfano, usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa.
   Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zenye changamoto zitakazowawezesha kutoa huduma jumuishi za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**
   Elimu inafaa kuwapa vijana uelewa wa tamaduni za kale na za sasa na nafasi yazo katika jamii ya kisasa. Vijana wanafaa kuambatanisha maadili ya tamaduni bora na mahitaji yanayobadilika kulingana na maendeleo yanayotokea ili kujenga jamii thabiti ya kisasa.

7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**
   Kenya kama nchi mojawapo ya jamii ya kimataifa inakusudia elimu iwaelekeze Wakenya kutambua na kuthamini mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia mikataba, uwajibikaji, haki na manufaa yanayoambatana na ushirika huo.

8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira**
   Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Aidha, inafaa kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira na kuwaelekeza vijana kuthamini usafi wa mazingira.

## MGAO WA VIPINDI KATIKA SHULE YA MSINGI DARAJA YA JUU

| S/ No. | Somo | Vipindi |
|---|---|---|
| 1. | English for Learners with Visual Impairment | 5 |
| 2. | Kiswahili for Learners with Visual Impairment | 4 |
| 3. | Mathematics for Learners with Visual Impairment | 5 |
| 4. | Religious Education | 3 |
| 5. | Science & Technology for Learners with Visual Impairment | 4 |
| 6. | Agriculture & Nutrition for Learners with Visual Impairment | 4 |
| 7. | Social Studies for Learners with Visual Impairment | 3 |
| 8. | Creative Arts for Learners with Visual Impairment | 6 |
| 9. | Pastoral/ Religious Instruction Programme | 1 |
| | **Jumla** | **35** |

**MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA ELIMU YA MSINGI**

Kufikia mwisho wa elimu ya msingi, mwanafunzi aweze:

a) kuwasiliana apasavyo akitumia mbinu za mazungumzo na ishara katika miktadha mbalimbali,
b) kutumikiza maarifa, ujuzi, maadili na mitazamo katika maisha ya kila siku,
c) kudhhihirisha ujuzi wa kijamii maadili, na maadili ya kidini kwa nia ya kuchangia kukua kwa jamii,
d) kukuza talanta kwa nia ya kujiendeleza na kujifanikisha,
e) kuafiti, kutumia, kulinda na kutunza mazingira kwa nia ya kujifunza na kwa maendeleo endelevu,
f) kutumia ujuzi wa kidijitali wenye teknolojia saidizi kujifunza na kujifurahisha,
g) kuthamini tamaduni mbalimbali kwa nia ya kuishi kwa amani,
h) kufurahia haja ya umuhimu wa kutegemeana kwa binadamu na mataifa.

**KAULI KIINI**

Mwanafunzi wa lugha ya Kiswahili aliye na changamoto za kuona katika shule ya msingi atajenga stadi na umahiri ufaao kuwasiliana, kutangamana na kushiriki katika miktadha mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa kutumia lugha kuzungumza na kuandika. Mwanafunzi aliye na changamoto za kuona anahitaji kujifunza kunga za Kiswahili ili kuitumia lugha hii kama wenzo wa ujifunzaji. Mwanafunzi asiyeona, pia anahitaji kujifunza kutumia alama za breli zifaazo na mikato ya breli ili kuimarisha uwezo wao wa kuandika na kusoma. Aidha, mwanafunzi hufunzwa Kiswahili ili kushiriki na kukichangamkia katika hali zake mbalimbali. Hili humwezesha kujenga stadi za kimsingi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Kwa kujifunza sarufi na matumizi ya Kiswahili kimuktadha, mwanafunzi anaweza kuwasiliana kwa ufasaha, umahiri na kwa namna ambayo itaimarisha utangamano darasani na katika ulimwengu mpana. Nadharia ya sarufi bia ya Noam Chomsky (1965), inaeleza kuwa binadamu ana uwezo asilia wa kuvimudu vipengele vya kisarufi. Uwezo huu huchangia katika ukuaji wa lugha wa mwanafunzi na hivyo kumfanya mzungumzaji stadi wa lugha anayeweza kubaini matumizi sahihi na yasiyo sahihi.

## MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI

Kufikia mwisho wa shule ya msingi, mwanafunzi aweze:

a) kusikiliza kwa makini na kuitikia ipasavyo kwa Kiswahili katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano

b) kuzingatia kanuni za lugha kuwasiliana kiubunifu kwa njia ya mazungumzo na maandishi

c) kujieleza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali

d) kusoma kwa ufasaha na kufahamu matini mbalimbali yaliyochapishwa na ya kidijitali na kutumia maarifa anayoyapata katika mazingira tofauti maishani

e) kutumia hati au nukta nundu zifaazo za kimaandishi na mfumo wa kidijitali wenye teknolojia saidizi kuwasiliana ipasavyo kwa kuzingatia mitindo na miundo husika katika miktadha mbalimbali

f) kuchangamkia matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa katika mawasiliano ya kila siku

**MADA**

1. Kusikiliza na Kuzungumza
2. Kusoma
3. Kuandika
4. Sarufi

**MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO**

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Muda Uliopendekezwa** |
|---|---|---|
| **Kusikiliza na Kuzungumza** | 1.1.1 Matamshi Bora | 2 |
| | 2.1.1 Maamkuzi na Maagano | 2 |
| | 3.1.1 Vitendawili | 2 |
| | 4.1.1 Maneno ya Upole | 2 |
| | 5..1 Methali | 2 |
| | 6.1.1Ushairi | 2 |
| | 7.1.1 Nahau | 2 |
| | 8.1.1Visawe | 2 |
| | 9.1.1.1Mazungumzo ya Kimuktadha | 2 |
| | 10.1.1 Tashbihi | 2 |
| | 11.1.1 Masimulizi | 2 |
| **Kusoma** | 1.2.1 Kusoma kwa Ufahamu | 2 |
| | 2.2.1 Kusoma kwa Kina | 2 |
| | 3.2.1 Kusoma kwa Ufasaha | 2 |
| | 4.2.1Kusoma kwa Mapana | 2 |
| | 5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu | 2 |

| | | |
|---|---|---|
| | 6.2.1Kusoma kwa Mapana | 2 |
| | 7.2.1 Kusoma kwa Mapana | 3 |
| | 8.2.1 Kusoma kwa Ufahamu | 2 |
| | 9.2.1 Kusoma kwa Mapana | 2 |
| | 10.2.1. Kusoma Kidijitali | 2 |
| | 11.2.1 Kusoma kwa Ufasaha | 2 |
| **Kuandika** | 1.3.1 Insha ya Wasifu, | 2 |
| | 2.3.1 Insha ya Masimulizi | 2 |
| | 3.3. Kuandika kwa Tarakilishi | 2 |
| | 4.3.1 Barua ya Kirafiki | 2 |
| | 5.3.1 Insha za Maelezo | 2 |
| | 6.3.1 Insha za Wasifu | 2 |
| | 7.3.1 Insha za Maelezo | 2 |
| | 8.3.1 nsha za Masimulizi | 2 |
| | 9.3.1 Kuandika Maelezo | 2 |
| | 10.3.1 Insha za Masimulizi | 2 |
| | 11.3.1 Barua ya Kirafiki | 2 |
| **Sarufi** | 1.4.1 Nomino | 2 |

| | | |
|---|---|---|
| | 1.4.2 Vitenzi | 2 |
| | 1.4.3 Vivumishi | 2 |
| | 2.4.1 Viwakilishi | 2 |
| | 2.4.2 Vielezi | 2 |
| | 3.4.1 Viunganishi | 2 |
| | 3.4.2 Vihusishi | 2 |
| | 3.4.3 Vihisishi | 2 |
| | 4.4.1 Ngeli ya A-WA | 4 |
| | 5.4.1 Ngeli ya U-I | 4 |
| | 6.4.1 Ngeli ya LI-YA | 4 |
| | 7.4.1 Ngeli ya KI-VI | 4 |
| | 8.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi | 4 |
| | 9.4.1 Vinyume vya Nomino | 3 |
| | 10.4.1 Nyakati na Hali | 4 |
| | 11.4.1 Ukanushaji | 3 |
| | 11.4.2. Ukubwa na Udogo wa Nomino | 2 |
| | 11.4.3 Udogo wa Nomino | 2 |
| | **Jumla ya Vipindi** | **120** |

**KUMBUKA:**
Idadi ya vipindi vilivyopendekezwa kwa kila mada ndogo vinaweza kuwa vichache au vingi kutegemea na muktadha.

**Matokeo ya Kijumla Yanayotarajiwa Katika Kiwango cha Pili cha Masomo**.

Kufikia mwisho wa kiwango cha pili cha masomo, mwanafunzi aweze:

a) kutumia mbinu zifaazo za usikivu katika mawasiliano kwenye mazingira yake,
b) kudhihirisha ufasaha wa kuzungumza kwa Kiswahili,
c) kusoma kwa ufasaha na kufahamu aina zozote za maandishi ya Kiswahili,
d) kuelezea mawazo, hisia na tajiriba kwa maandishi ya mkono au mbinu nyingine yoyote ya uwasilishaji,
e) kutumia sarufi ipasavyo katika mawasiliano,
f) kutumia msamiati ufaao katika mazingira yake kuwasiliana,
g) kuonyesha ukakamavu katika kuwasilisha masuala yanayomkabili na yanayokabili mazingira yake.

## 1.0 NYUMBANI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1.1 Matamshi Bora**<br>*Sauti*<br>● *p/b*<br>● *t/d*<br>● *k/g*<br>● *ch/j*<br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi zinazotokana na sauti p/b, t/d, k/g, ch/j katika maneno,<br>b) kutamka silabi zinazotokana na sauti p/b, t/d, k/g, ch/j,<br>c) kutamka vitanzandimi vinavyoundwa kwa silabi za sauti p/b, t/d, k/g, ch/j,<br>d) kuunda vitanzandimi kutokana na sauti p/b, t/d, k/g, ch/j,<br>e) kuchangamkia kukariri vitanzandimi vinavyoundwa kwa silabi za sauti | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua silabi za sauti, /p//b/, /t//d/, /k//g/, /ch//j/ kutokana na maneno kwenye vitabu, ubaoni au kwa kutumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi asikilize silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi k.v. kinasasauti na rununu.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutamka silabi za sauti lengwa na vitanzandimi akiwa peke yake au wakiwa na wenzake. | Kwa nini ni muhimu kutamka silabi ipasavyo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | zinazokaribiana kimatamshi katika kuboresha matamshi yake. | • Mwanafunzi asikilize vitanzandimi vinavyoundwa kutokana na maneno yenye sauti lengwa vikikaririwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.m. *baba alivua papa katika bahari pana, kila Chacha akila hali chakula kikichacha*),<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuunda vitanzandimi vyepesi vinavyotokana na vitate husika akiwa peke yake au wakiwa na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuunda vitanzandimi kwenye mitambo ya kidijitali yenye teknolojia saidizi na kushirikiana na wenzake mitamboni kuvirekebisha. | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi ashiriki majadiliano kuhusu sababu za kukariri vitanzandimi maishani mwake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala shuleni.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kusikiliza sauti.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoendelea kukariri vitanzandimi pia anapotoa muhtasari wa kifungu ili kupata kuelewa zaidi.
- Ubunifu: mwanafunzi anaposhiriki katika kuunda vitanzandimi.

**Maadili:**

- Umoja: wanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili maana na matumizi ya msamiati lengwa.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuunda vitanzandimi pamoja na wenzake.
- Uzalendo: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kutoka jamii mbalimbali katika kutamka silabi za sauti lengwa na vitanzandimi.

**Masuala Mtambuko:**

- Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka maeneo tofauti tofauti kuunda vitanzandimi kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kuvirekebisha.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili pia linashughulikia sauti zinazokaribiana kimatamshi.

| |
| --- |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Mgeni mwalikwa, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati wa mada lengwa uliotumika katika kifungu cha hadithi ili kuimarisha ufahamu,<br>b) kutumia msamiati lengwa kwa usahihi katika sentensi,<br>c) kutoa muhtasari wa ujumbe wa kifungu cha hadithi,<br>d) kujenga mazoea ya usomaji bora katika maisha ya kila siku. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua msamiati wa nyumbani (k.v. *meza*, *sebule*, *balbu/globu*, *kizingiti*, *fremu*, *neti*, *tendegu*, *mtoto wa meza*, *mvungu*, *figa*, *kinu*, *tumbuu*, *kochi*, *kupiga deki*) kwa kutumia kadi za maneno, michoro, chati na mti maneno.<br>● Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua msamiati wa nyumbani (k.v. *meza*, *sebule*, *balbu/globu*, *kizingiti*, *fremu*, *neti*, *tendegu*, *mtoto wa meza*, *mvungu*, *figa*, *kinu*, *tumbuu*, *kochi*, *kupiga deki*) kwa kutumia kadi za maneno za breli na michoro yenye maelezo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua msamiati wa nyumbani kwa kutumia | Mbona ni muhimu kutambua msamiati katika kifungu cha hadithi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | tarakilishi yenye teknolojia saidizi na projekta.<br>● Mwanafinzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchora na kuonyesha vifaa vya nyumbani kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kufinyanga na vifaa vya nyumbani na kusikiliza maelezo ya vifaa vya nyumbani kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kutumia herufi za breli zifaazo k.v /a/, /b/, /ch/, /d/.<br>● Mwanafunzi ashiriki katika vikundi kujadili maana na matumizi ya msamiati lengwa katika sentensi.<br>● Mwanafunzi aimbe nyimbo zinazolenga msamiati lengwa.<br>● Mwanafunzi asome kifungu kinachohusiana na mada lengwa kwenye kitabu au kwenye tarakilishi akiwa peke yake, wawili wawili au katika vikundi.<br>● Mwanafunzi atoe muhtasari kuhusu kifungu alichokisoma.<br>● Mwanafunzi aulize au ajibu maswali kutokana na kifungu alichosoma. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.<br>Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anatumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kusoma maneno.<br>Hamu ya ujifunzaji**:** mwanafunzi anapoyatafakari Swali Dadisi Lililopendekezwa. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anathamini maoni ya wenzake wanapojadili maana na matumizi ya msamiati lengwa katika sentensi.<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kusaidiana. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi au projekta kuchora au kutoa maelezo ya vifaaa vya nyumbani kwa uangalifu. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili pia lina stadi ya kusoma kwa ufahamu. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Tarakilishi yenye teknolojia saidizi, projekta, kadi maneno, michoro, michoro yenye maelezo, chati mti maneno |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Insha ya Wasifu**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya wasifu kwa kuzingatia muundo,<br>b) kuandika insha ya wasifu kwa kuzingatia ujumbe, mtindo na muundo ufaao,<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wa insha ya wasifu ili kujenga ubunifu wake. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua insha ya wasifu kwa kurejelea vielelezo vya insha vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aandae vidokezo vitakavyomwongoza kuandika insha yake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika insha daftarini inayoeleza sifa za mtu kama vile mzazi au mlezi, rafiki, mwalimu au kiongozi yeyote kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa ubunifu, mwanafunzi asiyeona aandike insha kwenye karatasi za breli inayoeleza sifa za mtu kama vile mzazi au mlezi, rafiki, mwalimu au kiongozi yeyote kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, nukta nundu zifaazo, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa ubunifu. | Je, unaweza kuandika insha nzuri ya wasifu kivipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya wasifu.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya wasifu mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili waisome na kuitathmini.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoiandika ili waitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi kujadili mada na muundo wa insha ya wasifu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika na kusambaza insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya wasifu.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya wasifu.
- Hamu ya ujifunzaji**:** mwanafunzi anapoyatafakari Swali Dadisi Lililopendekezwa na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi na vyombo vingine vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.

**Maadili:**

- Heshima: wanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili mada na muundo wa insha ya wasifu.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika insha na kukitunza.

**Masuala Mtambuko:**
Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapofanya shughuli za kikundi pamoja na wenzake kwa amani.
Haki za watoto: mwanafunzi anaposoma masuala kuhusu mambo ya nyumbani katika insha au kifungu.

| |
|---|
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili pia linashughulikia dhana ya kuandika insha ya wasifu. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli, kielelezo cha insha ya wasifu |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1 Nomino** (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya nomino ili kuitofautisha na aina nyingine za manenoc,<br>b) kutambua nomino katika kundi la maneno na sentensi,<br>c) kutumia nomino kwa njia sahihi katika sentensi,<br>d) kuonea fahari matumizi ya nomino katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kueleza maana ya nomino na kuzitungia sentensi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua nomino katika kundi la maneno aliyopewa.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kutoa mifano ya nomino.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona apewe maneno kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi, achague nomino na aziburure na kuzitia kapuni au aziorodheshe akiwa peke yake au kwenye vikundi, mwanafunzi asiyeona | Kwa nini ni muhimu kueleza maana ya nomino na kuitofautisha na aina nyingine za maneno? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>apewe orodha ya maneno ayaorodheshe na kuyaandika kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au kwenye vikundi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia nomino kutunga sentensi kwenye daftari na mtandaoni ili wenzake wazisome na kuzisahihisha, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia nomino kutunga sentensi kwenye karatasi za breli na mtandaoni ili wenzake wazisome na kuzisahihisha.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala, kazi za vikundi na mawasiliano mtandaoni.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi katika kutambua nomino na kutunga sentensi mtandaoni.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia nomino.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua nomino na kuzitungia sentensi sahihi.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>● Uadilifu: unakuzwa mwanafunzi anaposahihisha sentensi zilizoandikwa na mwenzake kwa uaminifu.<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kueleza maana ya nomino bila ubaguzi.<br>● Uzalendo: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kutoka jamii mbalimbali katika kutekeleza shughuli za kikundi.</td></tr>
</table>

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu masuala ya nyumbani. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili hushughulikia dhana ya nomino. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli, orodha maneno, kadi maneno |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.2 Vitenzi** (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya vitenzi ili kuvitofautisha na aina nyingine za maneno,<br>b) kutambua vitenzi katika kundi la maneno na sentensi,<br>c) kutumia vitenzi ipasavyo katika mawasiliano,<br>d) kuonea fahari matumizi ya vitenzi katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kueleza maana ya vitenzi na kuvitungia sentensi.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kutoa mifano ya vitenzi (*k.v. soma, andika, keti, simama, cheka).*<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vitenzi katika kundi la maneno aliyopewa kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi ili achague vitenzi, aviburure na kuvitia kapuni, | Unaweza kutambua vitenzi katika kundi la maneno na sentensi kivipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mwanafunzi asiyeona atambue vitenzi katika orodha ya maneno aliyopewa kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi ili achague vitenzi na aviorodheshe akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vitendo vinavyofanyika katika picha, mwanafunzi asiyeona aweze kutambua vitendo vinavyofanyika katika maelezo ya picha yaliyotolewa.<br>● Mwanafunzi aigize vitenzi mbalimbali akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia vitenzi kutunga sentensi na kujaza nafasi kwenye sentensi daftarini akiwa peke yake na vilevile akishirikiana na wenzake, mwanafunzi asiyeona atumie vitenzi kutunga sentensi na kujaza nafasi kwenye karatasi za breli akiwa peke yake na vilevile akishirikiana na wenzake. | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aelekezwe kutumia vitenzi kutunga sentensi mtandaoni ili wenzake wazisome na kuzisahihisha. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala, kazi za vikundi na mawasiliano mtandaoni.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi katika kutambua vitenzi na kutunga sentensi mtandaoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia vitenzi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua vitenzi na kuvitungia sentensi sahihi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu wenzake wanaposhiriki katika kutunga sentensi.

**Masuala Mtambuko:**

Haki za watoto: mwanafunzi anaposikiliza na kutunga sentensi kuhusu nyumbani na na masuala ya watoto.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili linashughulikia dhana ya vitenzi.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli, picha zinazoonyesha vitenzi, maelezo ya picha zinazoonyesha vitenzi

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.3 Vivumishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kivumishi ili kukitofautisha na aina nyingine za maneno,<br>b) kutambua vivumishi katika kundi la maneno na sentensi,<br>c) kutumia vivumishi ipasavyo katika sentensi na kifungu,<br>d) kuonea fahari matumizi ya vivumishi katika sentensi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vivumishi katika kundi la maneno aliyopewa (*k.m. -zuri, -baya, -refu, -fupi, -eusi, -eupe,).*<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kueleza maana ya vivumishi na kuvitungia sentensi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona apewe maneno kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi achague vivumishi, aviburure na kuvitia kapuni au ayaorodheshe akiwa peke yake au kwenye vikundi, mwanafunzi asiyeona apewe orodha ya maneno kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi achague vivumishi na aviorodheshe akiwa peke yake au kwenye vikundi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia vivumishi kutunga sentensi daftarini na mtandaoni ili wenzake wazisome na kuzisahihisha, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia vivumishi kutunga | Unaweza kutambua vivumishi mbalimbali kivipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | sentensi kwenye karatasi za breli na mtandaoni ili wenzake wazisome na kuzisahihisha.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuandika aya fupi akitumia vivumishi kueleza kitu, mtu, hali na mahali. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala, kazi za vikundi na mawasiliano mtandaoni.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi katika kutambua vivumishi na kutunga sentensi mtandaoni.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua vivumishi na kuvitungia sentensi sahihi.

**Maadili:**

- Heshima: mnakuzwa hasa katika shughuli za vikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake wanapotambua vivumishi katika kundi la maneno.

**Masuala Mtambuko:**
Utunzi na usalama wa watoto: mwanafunzi anapoingiliana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili linashughulikia dhana ya vivumishi..

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**
Tarakilishi yenye teknolojia saidizi, orodha maneno, vifaa vya breli,

## 2.0 NIDHAMU MEZANI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1 Maamkuzi na Maagano**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua aina mbalimbali za maamkuzi na maagano katika mawasiliano,<br>b) kueleza maamkuzi na maagano yanayotumika katika miktadha mbalimbali,<br>c) kutumia aina mbalimbali za maamkuzi na maagano katika mawasiliano,<br>d) kuchangamkia maamkuzi na maagano katika mahusiano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua maamkuzi (*k.v. U mzima? U hali gani? Alamsiki, Lala unono, Siku njema, Makiwa)* kutoka kwenye chati, ubao au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, michoro na picha, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua maamkuzi (*k.v. U mzima? U hali gani? Alamsiki, Lala unono, Siku njema, Makiwa)* kutoka kwenye orodha maneno, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, michoro yenye maelezo na picha zilizo na maelezo ya picha.<br>● Mwanafunzi ashiriki mjadala na mwenzake kuhusu maamkuzi na maagano yanayolengwa na matumizi yake. | Kwa nini ni muhimu watu kuamkuana na kuagana katika jamii yako? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kuigiza maamkuzi na maagano lengwa,<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atazame watu wakiamkuana na kuagana katika vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona asikilize watu wakiamkuana na kuagana katika vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi apewe orodha ya maamkuzi na maagano ili kuyaambatanisha na majibu sahihi<br>kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuigiza maamkuzi na maagano.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kujifunza maagano na maamkuzi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotumia maamkuzi na maagano ipasavyo.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoigiza maamkuzi na maagano.
- Upendo: mwanafunzi anaposhiriki katika mjadala na wenzake kwa kutumia maamkuzi na maagano yafaayo.
- Umoja: mnaimarishwa na uhusiano mwema mwanafunzi anapofanya shughuli za kikundi.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Elimu ya amani: mwanafunzi anapoamkuana na kuagana na wenzake.<br>● Umoja wa kijamii: mwanafunzi anapomuamkua na kumuaga mwenzake kutoka jamii tofauti. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia dhana ya maamkuzi na maagano. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Tarakilishi zenye teknolojia saidizi, picha, picha zenye maelezo, michoro, michoro yenye maelezo, chati, ubao |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.2 Kusoma** | **2.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kamusi ili kuitofautisha na vitabu vingine,<br>b) kutumia kamusi ipasavyo kutafuta maana za maneno asiyoyajua ili kukuza msamiati wake,<br>c) kuchangamkia umuhimu wa kamusi katika | ● Mwanafunzi ashiriki kujadiliana na wenzake kuhusu maana na matumizi ya kamusi.<br>● Mwanafunzi ajadiliane na wenzake kuhusu mpangilio wa maneno katika kamusi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atumie kamusi kutafuta maana za maneno mbalimbali akiwa peke yake, wawili wawili au katika vikundi. mwanafunzi | 1. Kwa nini ni muhimu kutumia kamusi?<br><br>2. Unatafutaje maneno kwenye kamusi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kukuza msamiati wake. | asiyeona atumie mtandao kutafuta maana za maneno mbalimbali akiwa peke yake, wawili wawili au katika vikundi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia mtandao kutafuta maana za maneno.<br>● Mwanafunzi atumie mtandao kusikiliza na kusoma maelezo kuhusu msamiati anaotafutia maana. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutafuta maana za maneno.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia mtandao kutafuta maana za maneno.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoanza kutumia kamusi kutafuta maana za maneno.

**Maadili:**
Uzalendo: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kutoka sehemu mbalimbali katika kutekeleza shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**
Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotumia mtandao kusikiliza na kusoma maelezo kuhusu msamiati asioujua.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili husisitiza matumizi mbalimbali ya kamusi.

| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kamusi mbalimbali, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |
|---|

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.3 Kuandika** | **2.3.1 Insha ya Masimulizi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya masimulizi kwa kuzingatia muundo,<br>b) kuandika insha ya masimulizi inayozingatia mada, ujumbe, mtindo na muundo ufaao,<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wa insha ya masimulizi ili kukuza ubunifu wake. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua insha ya masimulizi kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandaa vidokezo vitakavyomwongoza kuandika insha yake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha inayosimulia kisa kinachohusu nidhamu mezani kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu.<br>● Mwanafunzi ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya masimulizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya masimulizi mtandaoni na | 1. Mbona unazinatia vipengele vifuatavo katika Insha ya masimulizi?<br>2. Je, unaweza kuandika insha ya masimulizi kivipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili waisome na kuitathmini.<br>● Mwanafunzi asomee wenzake insha aliyoandika ili waitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya masimulizi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoyatafakari Swali Dadisi Lililopendekezwa na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi.

**Maadili**
Heshima: mwanafunzi anapothamini mchango wa wenzake katika kikundi.

**Masuala Mtambuko:**
Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapokuza uraia wema kwa kufanya shughuli ya kikundi na wenzake na kuthamini mchango wao.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili linashughulikia insha ya masimulizi

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Kielelezo cha insha ya masimulizi, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Viwakilishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kiwakilishi ili kukibainisha,<br>b) kutambua viwakilishi katika kundi la maneno na sentensi,<br>c) kutumia viwakilishi ipasavyo katika sentensi,<br>d) kuonea fahari matumizi ya viwakilishi katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kueleza maana ya viwakilishi na kuvitungia sentensi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua viwakilishi katika kundi la maneno aliyopewa.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona apewe maneno kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi achague viwakilishi, aviburure na kuvitia kapuni akiwa peke yake au kwenye vikundi, mwanafunzi asiyeona apewe orodha ya maneno kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi achague viwakilishi na aviorodheshe akiwa peke yake au kwenye vikundi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia viwakilishi kutunga sentensi daftarini na mtandaoni ili wenzake wazisome na | 1. Kwa nini ni muhimu kueleza maana ya viwakilishi?<br>2. Unatambua vipi viwakilishi katika kundi la maneno na sentensi, |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuzisahihisha, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia viwakilishi kutunga sentensi kwenye karatasi za breli na mtandaoni ili wenzake wazisome na kuzisahihisha.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi kwa kutumia viwakilishi mwafaka.<br>● Mwanafunzi awasomee au kuwasambazia wenzake sentensi zake ili kuzitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala, kazi za vikundi na mawasiliano mtandaoni.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi katika kutambua viwakilishi na kutunga sentensi mtandaoni.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua viwakilishi na kuvitungia sentensi sahihi.

**Maadili:**

- Amani: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za kikundi.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini mchango wa wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Elimu kwa maendeleo endelevu: mwanafunzi anapotumia viwakilishi ipasavyo katika mawasiliano ya kila siku.

| |
|---|
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia dhana ya viwakilishi. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli, |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.2 Vielezi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kielezi ili kukibainisha,<br>b) kutambua vielezi katika kundi la maneno au sentensi,<br>c) kutumia vielezi ipasavyo katika mawasiliano,<br>d) kuonea fahari matumizi ya vielezi katika sentensi. | ● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kueleza maana ya vielezi na kuvitungia sentensi *(k.v polepole, haraka, sana, vizuri, kisheria, jana, shuleni, uwanjani*).<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vielezi katika kundi la maneno aliyopewa katika kadi za maneno, chati, mti maneno, ubao, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua vielezi katika kundi la maneno aliyopewa katika orodha maneno,kadi za breli au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchagua | Unafanyaje shughuli zako za kila siku? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vielezi kutoka kwenye kundi la maneno kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuviburura na kuvitia kapuni akiwa peke yake au kwenye vikundi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchagua vielezi kutoka kwenye kundi la maneno kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi na kuviorodhesha akiwa peke yake au kwenye vikundi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuigiza vielezi mbalimbali panapofaa akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vitendo kwa maneno katika video na kuvitungia sentensi akitumia vielezi vifaavyo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia vielezi kutunga sentensi na kujaza nafasi kukamilisha sentensi kwa vielezi mwafaka.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia vielezi kutunga sentensi mtandaoni ili wenzake wazisome na kuzisahihisha. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala, kazi za vikundi na mawasiliano mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi katika kutambua vielezi na kutunga sentensi mtandaoni.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua vielezi na kuvitungia sentensi sahihi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafakari Swali Dadisi Lililopendekezwa na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anaposikiliza vielezi vinavyotolewa na wenzake kwa makini.<br>● Upendo: mwanafunzi anapoigiza akishirikiana na wenzake kwa zamu. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Haki za watoto: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa akizingatia vielezi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia dhana ya vielezi. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kadi za maneno, kadi za breli, chati, mti maneno, orodha maneno, ubao, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

## 3.0 MAVAZI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.1 Kusikiliza na kuzungumza** | **3.1.1 Vitendawili**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vitendawili kwenye matini,<br>b) kutega na kutegua vitendawili ili kukuza uwazaji kina,<br>c) kuchangamkia matumizi ya vitendawili maishani. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutafiti maana ya kitendawili kwenye kamusi, vitabuni au mtandaoni akiwa na wenzake,<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vitendawili katika chati, ubao au katika vifaa vya kidijitali *(k.m. Nifungue nikufunike (Mwavuli): Pitia huku nami nipitie kule, tupatane pale (mshipi): Ukinitembelea nyayo zi salama (viatu),* mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua vitendawili katika chati ya breli au katika vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi *k.m. Nifungue nikufunike (Mwavuli): Pitia huku nami nipitie kule, tupatane pale (mshipi): Ukinitembelea nyayo zi salama (viatu),*<br>● Mwanafunzi asikilize | Utatambua vipi vitendawili kwenye matini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vitendawili vikitegwa na kuteguliwa kupitia vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashiriki katika kutega na kutegua vitendawili akiwa na wenzake,<br>● Mwanafunzi ajadiliane na mzazi au mlezi wake kuhusu vitendawili vinavyotegwa katika jamii yao. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kutega na kutegua vitendawili kwenye vikundi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapofikiria kuhusu majibu ya vitendawili.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kutambua na kusikiliza vitendawili vikitegwa na kuteguliwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotega na kutegua vitendawili.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anachangamkia maoni ya wenzake darasani.
- Umoja: wanafunzi wanapofanya kazi ya kutega na kutegua vitendawili pamoja na wenzake kwa vikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Umoja wa kijamii: mwanafunzi anapofanya kazi ya kutega na kutegua vitendawili pamoja na wenzake katika kikundi.

| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>**English**: somo hili linashughulikia vitendawili. |
|---|
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Vifaa vya kiditali vyenye teknolojia saidizi, chati, chati za breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha,<br>b) kusoma kifungu cha hadithi kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu cha hadithi kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti,<br>d) kusoma kifungu cha hadithi kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu cha hadithi kwa kuambatanisha ishara zifaazo, | ● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kujadili vipengele vya kuzingatia katika kusoma makala kwa ufasaha,<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona asikilize na atazame mwalimu, mgeni mwalikwa, mwanafunzi mwenzake au video za watu wanaosoma makala kwa ufasaha (k.v. hotuba na habari), mwanafunzi asiyeona asikilize mwalimu, mgeni mwalikwa, mwanafunzi mwenzake au watu wanaosoma makala yaliyorekodiwa kwa ufasaha (k.v. hotuba na habari)<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona ajadili na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa | Kwa nini ni muhimu kusoma kifungu cha hadithi ukizingatia vipengele vilivyotajwa? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | ufasaha vilivyozingatiwa katika usomaji alioutazama, mwanafunzi asiyeona ajadili na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha vilivyozingatiwa katika usomaji aliousikiliza<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu cha hadithi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu cha hadithi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti (k.v. kiwango cha sauti na kiimbo).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu cha hadithi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno yasiyopungua 70 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi) ili wenzake wamtolee maoni.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo panapofaa anaposoma *(k.v. ishara za uso na mikono)* mwanafunzi asiyeona asome kifungu kwa kutumia toni ifaayo anaposoma. | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma hadithi kuhusu masuala mtambuko mbalimbali kutoka kwenye vitabu, vifaa vya kidijtali vyenye teknolojia saidizi, n.k akizingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kiwango kifaacho cha sauti. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma hadithi kuhusu masuala mtambuko mbalimbali kutoka kwenye vitabu vya breli, vifaa vya kidijtali vyenye teknolojia saidizi n.k akizingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kiwango kifaacho cha sauti. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kusoma kifungu cha hadithi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusoma vifungu cha hadithi kuhusu masuala mtambuko mbalimbali.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposhiriki mijadala darasani na kujibu maswali kwa usahihi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafuta hadithi mbalimbali na kuzisoma kwa kuzingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kiwango kifaacho cha sauti.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma kifungu cha hadithi.
- Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Stadi za maisha: mwanafunzi anapomudu kuzitumia sauti lengwa ipasavyo, ukakamavu wake unajengeka.<br>• Uraia: mwanafunzi anapowathamini wenzake wanaposhirikiana kutamka sauti lengwa katika kikundi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili pia linashughulikia kusoma kwa ufasaha. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kadi za maneno, kadi za breli, michoro, maelezo ya michoro,chati, mti maneno, video, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Kuandika kwa Tarakilishi**<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sehemu mbalimbali za tarakilishi zinazotumika kupigia chapa,<br>b) kufungua na kufunga tarakilishi ili kuandika kazi na kuihifadhi,<br>c) kuandikia suala lengwa kwa kutumia tarakilishi,<br>d) kuhariri kazi yake kwa kuzingatia uakifishaji ufaao, | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua sehemu za kimsingi za tarakilishi za kupigia chapa akiwa na wenzake (k.v. *kiibodi, kipanya, kiwambo, kitufe* na *faili*), Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua sehemu za kimsingi za tarakilishi za kupigia chapa akiwa na wenzake kwa njia ya kupapasa (k.v. *kiibodi, kipanya, kiwambo, kitufe* na *faili*).<br>• Mwanafunzi azingatie hatua za kufungua na kufunga | Mbona unatambua sehemu mbalimbali za tarakilishi kabla ya kupiga chapa? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e) kuhifadhi kazi aliyoiandika kwenye tarakilishi,<br>f) kujenga mazoea ya kuandika kwa kutumia tarakilishi na kuhifadhi kazi yake ya maandishi. | tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika suala lengwa kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi akizingatia chapa koza, italiki na kupigia mistari panapofaa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika aya kuhusu mavazi katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi na kuihariri.<br>● Mwanafunzi aelekezwe atumie mtandao kusambaza kazi aliyoandika ili kuitathmini na kuiimarisha.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuhifadhi kazi yake kwenye faili ya tarakilishi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi kuandika na kuhifadhi kazi yake kwenye faili.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotagusana na vyombo vya kidijitali kama vile kutumia tarakilishi, kipakatalishi n.k.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Ushirikiano: unakuzwa anapotambua sehemu za kimsingi za tarakilishi za kupiga chapa akiwa na wenzake.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anaweza kutumia na kuhifadhi vyombo vya kidijitali ifaavyo. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Usalama wa mtandaoni: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi anazingatia kuingia mitandao iliyo salama. |
| **Uhusiano wa masomo mengine**<br>Science and Technology na English: masomo haya vilevile yanahimiza matumizi ya tarakilishi. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, nyenzo halisi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1 Viunganishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kiunganishi ili kukibainisha,<br>b) kutambua viunganishi katika kundi la maneno na sentensi,<br>c) kutumia viunganishi kwa njia sahihi katika mawasiliano,<br>d) kuonea fahari matumizi ya viunganishi katika sentensi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua viunganishi katika kundi la maneno aliyopewa (*k.v. na, pia, kwa sababu, lakini*).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutafiti vitabuni au mtandaoni ili kutoa mifano mbalimbali ya viunganishi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchagua viunganishi kutoka kwenye kundi la maneno yaliyo kwenye tarakilishi, aviburure na kuvitia kapuni akiwa peke yake au kwenye vikundi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchagua viunganishi kutoka kwenye kundi la maneno na aandike orodha hiyo ya maneno kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Katika vikundi, mwanafunzi ashirikiane na wenzake kueleza maana ya viunganishi na kuvitungia sentensi,<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia viunganishi kutunga sentensi daftarini au mtandaoni kwa | Je, kwa nini ni muhimu kutumia viunganishi katika mawasiliano? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuzingatia suala lengwa na masuala mtambuko mbalimbali, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia viunganishi kutunga sentensi kwenye kartasi za breli au mtandaoni kwa kuzingatia suala lengwa na masuala mtambuko mbalimbali.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi wake sentensi alizozitunga. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala, kazi za vikundi na mawasiliano mtandaoni.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi katika kutambua viunganishi na kutunga sentensi mtandaoni.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua viunganishi na kuvitungia sentensi sahihi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafakari Swali Dadisi Lililopendekezwa na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kueleza maana ya viunganishi na kuvitungia sentensi.
- Uadilifu: mwanafunzi anapotumia chombo cha kidijitali chenye teknologia saidizi kuchagua viunganishi kutoka kwenye kundi la maneno na kuvitia kapuni.

**Masuala Mtambuko:**
Umoja wa kijamii**:** mwanafunzi anapofanya shughuli ya kikundi pamoja na wenzake wa jamii tofauti.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili linashughulikia dhana ya viunganishi.

| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia** |
|---|
| Kapu la maneno, orodha maneno, kadi za breli, vifaa vya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.2 Vihusishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kihusishi ili kukibainisha,<br>b) kutambua vihusishi katika kundi la maneno na sentensi,<br>c) kutumia vihusishi ipasavyo katika sentensi,<br>d) kuonea fahari matumizi ya vihusishi katika mawasiliano. | • Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kueleza maana ya vihusishi na kuvitolea mifano (k.m. *karibu na*, *mbali na*, *juu ya*, *chini ya*, *nje ya* na *ndani ya*).<br>• Mwanafunzi atambue vihusishi katika kundi la maneno aliyopewa.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia vihusishi kutunga sentensi kwenye daftari akiwa peke yake au akishirikiana na wenzake, mwanafunzi asiyeona atumie vihusishi kutunga sentensi kwenye karatasi za breli.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchagua vihusishi kwenye kundi la maneno katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi, aviburure na kuvitia kapuni akiwa | Utatumia vipi vihusishi katika mawasiliano? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | peke yake au kwenye vikundi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuorodhesha vihusishi kutoka kwenye orodha maneno katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia vihusishi kutunga sentensi mtandaoni ili wenzake wazisome na kuzitathmini.<br>● Mwanafunzi awasomee au awasambazie wenzake na mwalimu sentensi alizotunga ili kuzitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala, kazi za vikundi na mawasiliano mtandaoni.
- Ujuzi wa kidijitali: wanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali teknolojia saidizi katika kutambua vihusishi na kutunga sentensi mtandaoni.
- Kujiamini:mwanafunzi anapofaulu kutambua vihusishi na kuvitungia sentensi sahihi.

**Maadili:**

- Heshima: Mwanafunzi anapothamini mchango wa wenzake katika kikundi.
- Uwajibikaji: Unakuzwa mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknologia saidizi  katika kutambua vihusishi na kuvitungia sentensi mtandaoni.

**Masuala Mtambuko:**
Umoja wa kijamii: mwanafunzi anapofanya shughuli ya kikundi pamoja na wenzake wa jamii tofauti.

| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia dhana ya vihusishi. |
|---|
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Tarakilishi yenye teknolojia saidizi, Orodha maneno, kadi za breli, vifaa vya breli. |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.3 Vihisishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kihisishi ili kukibainisha,<br>b) kutambua vihisishi katika kundi la maneno na sentensi,<br>c) kutumia vihisishi ipasavyo katika sentensi,<br>d) kuonea fahari matumizi ya vihisishi katika miktadha mbalimbali. | • Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kueleza maana ya vihisishi na kuvitolea mifano (k.m. *Lo! Ala!*, *Salalee!*, *Mama ee!*, *Oyee!* na *Aha!*).<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutambua vihisishi katika kundi la maneno aliyopewa.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutambua alama ya hisi (!) inayoambatanishwa na vihisishi,<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atumie vihisishi kutunga sentensi kwenye daftari akiwa peke yake au akishirikiana na wenzake, mwanafunzi asiyeona atumie vihisishi | Je, kwa nini ni nuhimu kutumia vihisishi katika mawasiliano? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kutunga sentensi kwenye karatasi za breli akiwa peke yake au akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchagua vihisishi kwenye kundi la maneno katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi, aviburure na kuvitia kapuni akiwa peke yake au kwenye vikundi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchagua vihisishi kwenye orodha maneno na ayaandike katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia vihisishi kutunga kifungu kifupi daftarini au mtandaoni ili wenzake wakisome na kukitathmini. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia vihisishi kutunga kifungu kifupi kwenye karatasi ya breli au mtandaoni ili wenzake wakisome na kukitathmini | |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala, kazi za vikundi na mawasiliano mtandaoni.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi unapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kutambua vihisishi na kutunga sentensi.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua vihisishi na kuvitungia sentensi sahihi. |
| **Maadili:**<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapochagua vihisishi kwenye kundi la maneno katika tarakilishi na kuvitia kapuni.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kueleza maana ya vihisishi na kuvitolea mifano. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Umoja wa kijamii: mwanafunzi anapofanya shughuli ya kikundi pamoja na wenzake wa jamii tofauti.<br>• Uwazaji wa kina: mwanafunzi anapotumia vihisishi kutunga sentensi mtandaoni ili wenzake wazitathmini. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia dhana ya vihisishi. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Tarakilishi yenye teknolojia saidizi, orodha maneno, vifaa vya breli**.** |

## 4.0 DIRA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.1 Kusikiliza na kuzungumza** | **4.1.1 Maneno ya upole**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno ya upole yanayotumiwa katika mawasiliano,<br>b) kutumia maneno ya upole katika mawasiliano,<br>c) kuthamini matumizi ya maneno ya upole katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua na aeleze maana ya maneno ya upole (k.m. *kwenda msalani*, *kwenda haja kubwa*, *kwenda haja ndogo*, *kuendesha*, *makalio*, *sehemu za siri* na *kujifungua*) katika chati, mti maneno, kapu maneno, ubao zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza, vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua na aeleze maana ya maneno ya upole (k.m. *kwenda msalani*, *kwenda haja kubwa*, *kwenda haja ndogo*, *kuendesha*, *makalio*, *sehemu za siri* na *kujifungua*) katika chati, mti maneno, kapu maneno, ubao zilizo na maandishi ya | 1. Mbona ni muhimu kutumia maneno ya upole katika mawasiliano?<br><br>2. Utashiriki vipi katika kujadili maneno ya upole? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | breli, vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashiriki katika kujadili maneno ya upole wakiwa wawili wawili na katika vikundi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atazame maigizo kuhusu matumizi ya maneno ya upole katika video na mitandaoni, mwanafunzi asiyeona asikilize maigizo kuhusu matumizi ya maneno ya upole katika video na mitandaoni.<br>● Mwanafunzi ashiriki katika maigizo yanayohusu matumizi ya maneno ya upole.<br>● Mwanafunzi atumie maneno ya upole katika sentensi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: wanafunzi wanapojadiliana na kuigiza katika vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika ujifunzaji.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua maneno ya upole na kuyatumia katika kutunga sentensi.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapotambua na kutumia maneno ya upole katika chati maneno au orodha maneno.<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika vikundi kwa amani. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Umoja wa kijamii: mwanafunzi anapojadiliana na kushirikiana na wenzake katika shughuli za vikundi kwa upole na amani. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English na Religious Education: lugha ya upole hufunzwa katika masomo haya. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>chati/kadi za breli, mti maneno, kapu maneno, orodha maneno, ubao, vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4.2.1 Kusoma kwa Mapana**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma,<br>b) kutambua na kuzingatia hatua za kiusalama katika matumizi ya vifaa vya kidijitali,<br>c) kusakura matini kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma vyenye mada lengwa,<br>d) kutumia vifaa vya kidijitali kwa urahisi kupata matini yanayolengwa,<br>e) kuchangamkia matumizi ya vifaa vya kidijitali katika kutafuta na kusoma ujumbe ili kuimarisha maarifa yake. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua na kuzingatia hatua za kiusalama (*k.m. kutowasiliana na watu asiowajua, kuwajibika anaposakura tovuti mbalimbali*) kutoka kwenye chati au kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi na mitandao.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua jina la faili lengwa kwenye tarakilishi na kufanya mazoezi ya kufungua na kufunga.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua mitandao salama yenye matini inayoafiki kiwango na mahitaji yake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua umuhimu wa kutoa habari kwa mwalimu, mzazi au mlezi wake endapo atapata ujumbe kutoka kwa watu asiowajua mtandaoni na kutowasiliana nao.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutafuta maana za maneno kuhusu mada lengwa (*k.m. kaskazini, kusini, magharibi, mashariki, kaskazini mashariki, kaskazini* | Kwa nini ni muhimu kuzingatia hatua za kiusalama unapotumia mtandao? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | *magharibi, kusini mashariki na kusini magharibi*) kwenye kamusi mtandaoni.<br>● Mwanafunzi asikilize matamshi na maelezo kuhusu anachokisoma mtandaoni panapowezekana.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutoa habari kuhusu matini aliyosoma kwa muhtasari na kujibu maswali katika maandishi au mazungumzo na wenzake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi katika kutafuta, kusakura na kusoma.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafuta matini ya kusoma kwenye tarakilishi na mitandaoni.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi na kuzingatia mitandao salama.
- Uadilifu: mwanafunzi anapotoa habari kwa mwalimu au mlezi apatapo ujumbe kutoka kwa watu asiowajua mtandaoni

**Masuala Mtambuko:**
Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotambua mitandao salama yenye matini inayoafiki kiwango na mahitaji yake.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- English: somo hili linashughulikia kusoma kwa mapana.
- Science and Technology: somo hili linafunza matumizi ya vifaa vya kidijitali.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, nyenzo halisi, muundo wa dira,picha ya dira, maelezo ya picha ya dira

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1 Barua ya Kirafiki**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua barua ya kirafiki kwa kuzingatia muundo wake,<br>b) kuandika barua ya kirafiki inayozingatia mada kwa kufuata kanuni zifaazo,<br>c) kuandika alama za breli za uakifishaji (mwanafunzi asiyeona)<br>d) kueleza umuhimu wa barua ya kirafiki katika mawasiliano,<br>e) kuchangamkia utunzi wa barua ya kirafiki katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua barua ya kirafiki kwa kurejelea vielelezo vya barua za kirafiki zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandaa vidokezo vitakavyomwongoza kuandika insha yake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika barua ya kirafiki kwa rafiki, ndugu, mzazi, n.k. daftarini kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika barua ya kirafiki kwa rafiki, ndugu, mzazi, katika karatasi ya breli kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, nukta nundu zifaazo, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka k.v koma,kikomo, na kwa lugha ya kiubunifu. | 1. Je, mbona ni muhimu kuzingatia kanuni zifaazo unapoandika barua ya kirafiki?<br>2. Unatambuaje barua ya kirafiki kuzingatia muundo wake? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi ajadiliane na wenzake mada ya barua ya kirafiki na vipengele vyake vinavyofaa kujumuishwa.<br><br>• Mwanafunzi aelekezwe kushirikisha msamiati wa mada lengwa (dira) katika barua yake.<br>• Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kujadili mada ya barua ya kirafiki na vipengele vyake/ yale yanayofaa kujumuishwa,<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuandika barua ya kirafiki mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili waisome na kuitathmini,<br>• Mwanafunzi awasomee wenzake na mwaimu barua yake ili waitathmini.<br>• Mwanafunzi ashirikiane na wenzake katika vikundi kujadili umuhimu wa barua za kirafiki<br>katika mawasiliano. | |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:** | | | | |

| |
| --- |
| • Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika barua za kirafiki.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kuandika barua ya kirafiki kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi au nukta nundu zifaazo, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu. |
| **Maadili:**<br>• Upend**o**: mwanafunzi anapoisambaza kazi aliyoifanya mtandaoni kwa wenzake ili waitathmini.<br>• Heshima: mwanafunzi anapojadili umuhimu wa kuandika barua za kirafiki kwa kuheshimu maoni ya wengine. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake wa jamii tofauti tofauti kujadili umuhimu wa barua za kirafiki katika mawasiliano. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia uandishi wa barua ya kirafiki. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kielelezo cha barua ya kirafiki, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya kuandikia breli, vitabu vyenye fonti zifaazo |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.1 Ngeli ya A-WA**<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya A-WA,<br>b) kutambua nomino katika ngeli ya A-WA ili kuzitofautisha na nomino katika ngeli nyingine,<br>c) kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya A-WA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi,<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya A-WA katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya ngeli za nomino akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutaja mifano ya nomino akiwa na wenzake<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya A-WA katika umoja na wingi,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya A-WA kwenye sentensi alizosoma,<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kushiriki katika mchezo wa kuchopoa kadi za sentensi zenye nomino za ngeli ya A-WA kutoka kwenye kikapu au boksi na kisha | Utawezaje kutambua nomino za ngeli ya A-WA zinazorejelea viumbe? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuzisoma, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchagua sentensi zenye nomino za ngeli ya A-WA kutoka kwenye orodha ya sentensi na kisha kuzisoma.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua nomino za ngeli ya A-WA katika umoja na wingi katika matini,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi katika sentensi kwa kutumia viambishi vya umoja na wingi wa nomino katika ngeli ya A-WA.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuunda sentensi sahihi daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akitumia nomino za ngeli ya A-WA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuunda sentensi sahihi kwenye karatasi za breli au kwenye kifaa cha kidijitali chenye | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | teknolojia saidizi akitumia nomino za ngeli ya A-WA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi.<br>● Mwanafunzi awasomee au kuwasambazia wenzake na mwalimu sentensi alizozitunga ili kuzitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika na kuandika nomino za ngeli ya A-WA katika umoja na wingi. Pia anaposhirikiana na wenzake katika mchezo wa kuchopoa kadi za sentensi zenye nomino za ngeli ya A-WA kutoka kikapuni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia nomino za ngeli ya A-WA katika umoja na wingi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapowaza kwa kina kuhusu mifano ya nomino.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi kutambua nomino.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza kifaa cha kidijitali anachotumia.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini mchango wa wenzake katika kuandika maneno ya ngeli ya A-WA.
- Amani: mwanafunzi anapowasiliana na wenzake kutoka sehemu mbalimbali kwa kuonyesha upendo akitumia nomino za ngeli ya A-WA.

**Masuala Mtambuko:**
Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapozingatia hatua za kiusalama kutambua nomino za ngeli ya A-WA kwenye tarakilishi.

| |
|---|
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linafundisha dhana ya ngeli za nomino. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Orodha maneno, mti maneno, kadi maneno, kadi za breli, kapu maneno, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

## 5.0 USHAURI-NASAHA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswaali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Methali:** Methali zinazohusu Malezi<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua methali katika matini tofauti tofauti,<br>b) kueleza maana za methali kuhusu malezi,<br>c) kutumia methali zinazohusu malezi katika mawasiliano,<br>d) kuchangamkia matumizi ya methali katika miktadha mbalimbali. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua methali kuhusu malezi (k.v. *mtoto umleavyo ndivyo akuavyo, mtoto wa nyoka ni nyoka* na *mtoto hutazama kisogo cha nina*) kutoka kwa kundi la methali,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana za methali kuhusu malezi akiwa na wenzake,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kukamilisha methali kuhusu malezi,<br>● Mwanafunzi aelekezwe | 1. Unawezaje kutambua methali zinazohusu malezi?<br>2. Mbona unatumia mehali kuhusu malezi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kutumia methali kuhusu malezi katika kifungu kifupi na masimulizi akiwa na wenzake<br>● Mwanafunzi aelekezwe kushirikiana na mzazi au mlezi wake kutambua methali kuhusu malezi katika jamii yao. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapohusishwa katika kazi ya vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia mtandao kutambua methali.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotumia methali kujieleza.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutaja na kueleza maana za methali na kuthamini mchango wao.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapowasiliana na mzazi au mlezi akitumia methali zinazohusu malezi katika miktatha mbalimbali.

**Masuala Mtambuko:**

- Ushauri nasaha: mwanafunzi anaposoma methali zinazohusu malezi mema.
- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake wa sehemu mbalimbali kueleza maana za methali kuhusu malezi kwa amani.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili linashughulikia dhana ya methali.

| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Tarakilishi yenye teknolojia saidizi, kamusi ya methali, vifaa vya breli |
|---|

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu:**<br>● *Ushairi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya shairi, ubeti na mshororo ili kuvibainisha,<br>b) kusoma shairi kwa ufasaha kwa kuzingatia ujumbe,<br>c) kutambua beti na mishororo katika shairi,<br>d) kutambua shairi kutokana na umbo lake,<br>e) kufurahia kutumia lugha ya ushairi anapozungumzia ushairi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua shairi, beti na mishororo katika matini mbalimbali kama vile vitabu, chati na vilevile kwa kutumia tarakilishi lenye teknologia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashiriki katika majadiliano kuhusu maana za shairi, ubeti na mishororo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma akizingatia msamiati wa mada lengwa.<br>● Mwanafunzi asikilize mashairi yanayokaririwa kwenye vifaa vya kidijitali vyenye teknologia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma au kukariri shairi kwa mahadhi mbalimbali akizingatia ujumbe. | 1. Kwa nini ni muhimu kusoma shairi kwa kuzingatia ujumbe?<br><br>2. Unaweza kuwasilisha mashairi kipivi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi ashiriki mjadala kuhusu ujumbe unaojitokeza kwenye shairi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusoma mashairi kwenye mitandao. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kufanikisha somo.
- Kujiamini:mwanafunzi anapoimba au kukariri shairi.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikikiana na wenzake katika majadiliano yanayohusu shairi bila ubaguzi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kufanikisha somo kwa uangalifu.

**Masuala Mtambuko:**

Masuala ya kijinsia: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake kusoma na kukariri mashairi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

English, Creative Arts na Religious Education: masomo haya yanashughulikia nyimbo na ushairi.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Nakala ya shairi, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vitabu vya breli/vyenye fonti zifaazo

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1 Insha ya Maelezo**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vifungu vya maelezo katika matini,<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kufuata kanuni zifaazo,<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wa insha ya maelezo ili kujenga ubunifu wake. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vifungu vya maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandaa vidokezo vitakavyomwongoza kuandika insha yake.<br>● Mwanafunzi aelkezwe kuandika insha ya maelezo kuhusu mada lengwa (ushauri-nasaha) akitumia vivumishi na vielezi vifaavyo kutoa picha dhahiri kuhusu anachokielezea akizingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu.<br>● Mwanafunzi ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya maelezo.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika insha ya maelezo daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kuwasomea au | 1. Unatambua vipi vifungu vya maelezo katika matini?<br>2. Mbona ni muhimu kufuata kanuni zifaazo unapoandika insha ya maelezo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuwasambazia wenzake na mwalimu ili kuitathmini, mwanfaunzi asiyeona aelekezwe kuandika insha ya maelezo kwenye karatasi ya breli au kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknoljia saidizi na kuwasomea au kuwasambazia wenzake na mwalimu ili kuitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika na kusambaza insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya maelezo.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo.

**Maadili:**

- Uadilifu: mwanafunzi anapotumia kifaa kidijitali chenye teknolojia saidizi uandika na kusambaza kazi yake mtandaoni kwa uangalifu.
- Upendo: mwanafunzi anapojitolea kuwasomea wenzake insha aliyoiandika ili kuitathmini.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika majadiliano ya mada na muundo wa insha ya maelezo kwa utulivu.

**Masuala Mtambuko:**
Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anapofanya shughuli ya kujadili mada na muundo wa insha ya maelezo pamoja na wenzake.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili linafundisha uandishi wa insha za maelezo.

| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia** |
|---|
| Kielelezo cha insha ya maelezo, vifaa vya kidijitali yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1 Ngeli ya U-I**<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya U-I,<br>b) kutambua nomino katika ngeli ya U-I ili kuzitofautisha na nomino katika ngeli nyingine,<br>c) kuunda sentensi akitumia nomino za ngeli ya U-I, katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi,<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya U-I katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kusoma sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya U-I katika umoja na wingi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya U-I kwenye sentensi alizosoma.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kushiriki katika mchezo wa kuchopoa kadi za sentensi zenye nomino za ngeli ya U-I kutoka kwenye kikapu au boksi na kisha kuzisoma. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kushiriki katika mchezo wa kuchagua sentensi zenye nomino za ngeli ya U-I kutoka kwenye orodha ya sentensi na kisha kuzisoma.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa | Kwa nini unatambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya U-I? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya U-I kwenye kadi, mti maneno, tarakilishi au kapu maneno, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya U-I kwenye kadi za breli, orodha ya nomino au kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi katika sentensi kwa kutumia viambishi vya umoja na wingi wa nomino katika ngeli ya U-I.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuunda sentensi sahihi daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali akitumia nomino za ngeli ya U-I katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuunda sentensi sahihi kwenye karatasi ya breli au kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akitumia nomino za ngeli ya U-I katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuwasomea au kuwazambazia wenzake na mwalimu sentensi alizozitunga ili kuzitathmini. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika vikundi kuandika nomino za ngeli ya U-I katika umoja na wingi.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kwa kutumia nomino za ngeli ya U-I katika umoja na wingi.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapowaza kwa kina kuhusu nomino zilizo katika ngeli ya U-I.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi kutunga sentensi na kuwasambazia wenzake na mwalimu. |
| **Maadili:**<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza tarakilishi na vifaa vingine anavyotumia.<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kuorodhesha nomino kuhusu suala lengwa.<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapozingatia hatua za kiusalama kutambua nomino za ngeli ya U-I kwenye tarakilishi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linafundisha dhana ya ngeli za nomino. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Orodha maneno, mti maneno, kadi maneno, kadi za breli, kapu maneno, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

## 6.0 BENDERA YA TAIFA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1** Shairi<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kukariri au kuimba shairi kwa kuzingatia matamshi na mahadhi mbalimbali,<br>b) kueleza maana ya msamiati uliotumiwa katika shairi,<br>c) kutumia msamiati uliotumiwa katika shairi ili kuboresha mawasiliano,<br>d) kueleza ujumbe wa shairi ili kudhihirisha ufahamu wake,<br>e) kuchangamkia ushairi kama njia ya kujieleza kwa ufasaha. | • Mwanafunzi aelekezwe kukariri shairi kuhusu mada lengwa (bendera ya taifa) kwa kuzingatia matamshi na mahadhi mbalimbali.<br>• Mwanafunzi asikilize shairi lengwa likikaririwa au kuimbwa na mwalimu, mgeni mwalikwa (mghani) au kupitia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kukariri au kuimba shairi kwa mahadhi mbalimbali.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutambua msamiati uliotumika katika ushairi kuhusu maadili (k.v. *uhuru, bendera, rangi za bendera, kupandisha* na *kushukisha bendera*) na kueleza akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wenzake.<br>• Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kujadili ujumbe katika shairi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kujibu maswali yanayotokana na shairi alilosikiliza, aliloimba au kukariri. | Mbona ni muhimu kukariri au kuimba shairi kwa kuzingatia matamshi na mahadhi mbalimbali? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za vikundi kukariri na kuimba shairi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposikiliza shairi lililorekodiwa likikaririwa kupitia vyombo vya kidijitali.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapojenga umilisi huu anapokariri shairi. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili ujumbe na matukio katika shairi na kuheshimu mchango wao.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anaposhiriki majukumu tofauti tofauti katika vikundi na kufuata mafunzo katika shairi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kitaifa: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kukariri shairi kuhusu bendera ya taifa kwa mahadhi na kutambua msamiati uliotumika. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>● English: somo hili linashughulikia ushairi.<br>● Creative Arts: Somo hili hushughulikia nyimbo na mashairi yenye mahadhi mbalimbali. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Nakala ya shairi, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Mapana**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kusoma makala kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vinavyoyajenga,<br>b) kusoma na kutambua umuhimu wa ujumbe wa makala husika,<br>c) kufurahia kusoma makala mbalimbali ili kukuza ufahamu. | ● Mwanafunzi aelekezwe kusoma makala ya aina mbalimbali (k.m. *hadithi fupi*, *michezo mifupi*, *mashairi mafupi*) akizingatia vipengele kama vile tahajia, sarufi, wahusika na ujumbe kutoka kwa kitabu, gazeti au blogi.<br>● Mwanafunzi ajadiliane na wenzake kuhusu makala aliyoyasoma na umuhimu wake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia kamusi kupata maana za msamiati uliotumika katika makala, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia mtandao kutafuta maana za msamiati uliotumika katika makala. | Kwa nini ni muhimu kusoma hadithi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposoma makala katika blogi.
- Kujiamini: mwanafunzi anajenga umilisi huu anaposimulia na kujadili na wengine alichokisoma.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotumia kamusi kupata maana za msamiati mpya uliotumika katika Makala.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu makala aliyoyasoma na umuhimu wake.<br>● Uzalendo**:** mwanafunzi anaposoma makala kuhusu jamii mbalimbali na kuheshimu mafunzo yanayojitokeza. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili kuhusu makala aliyoyasoma na umuhimu wake.<br>● Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapozingatia hatua za kiusalama anaposoma makala ya blogi mtandaoni. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Social Studies na English: uraia mwema na uzalendo unafundishwa katika masomo haya. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli, nakala ya gazeti. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1: Insha ya Wasifu**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya wasifu kwa kuzingatia muundo,<br>b) kuandika insha ya wasifu kwa kufuata kanuni zifaazo akizingatia vivumishi na vielezi kujenga picha dhahiri ya anachokielezea,<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wa kuandika insha ya wasifu ili kukuza ubunifu. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua insha ya wasifu kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandaa vidokezo vitakavyomwongoza kuandika insha yake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika insha inayoeleza sifa za mtu kama vile mzazi au mlezi, rafiki, mwalimu au kiongozi yeyote (kwa kutumia vivumishi na vielezi ili kujenga picha dhahiri ya anachokiandikia) daftarini kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika insha inayoeleza sifa za mtu kama vile mzazi au mlezi, rafiki, mwalimu au kiongozi yeyote kwenye karatasi za breli.<br>● Mwanafunzi ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya wasifu.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya wasifu mtandaoni na kuisambaza kwa | Unaweza kuandika vipi Insha ya wasifu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wenzake na mwalimu ili waisome na kuitathmini.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika ili waitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapovitumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya wasifu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoyatafakari Swali Dadisi Lililopendekezwa na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanfunzi anaposhirikiana na wenzake katika kufanikisha shughuli za kikundi kwa kuthamini maoni yao.
- Upendo: mwanafunzi anapojitolea kuisambaza insha yake mtandaoni ili mwalimu au wenzake waithamini.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika insha mtandaoni.

**Masuala Mtambuko:**
Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anapoandika insha yake mtandaoni na kujitolea kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili waisome na kuitathmini.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- English: somo hili pia hushughulikia uandishi kama mojawapo ya stadi za lugha.
- Social Studies: somo hili hushughulikia uraia na uzalendo.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Kielelezo cha insha ya wasifu, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Ngeli ya LI- YA**<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya LI-YA,<br>b) kutambua nomino katika ngeli ya LI -YA ili kuzitofautisha na nomino katika ngeli nyingine,<br>c) kuunda sentensi akitumia nomino za ngeli ya LI-YA, katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi,<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya LI-YA katika mawasiliano. | ● Mwanafaunzi aelekezwe kusoma sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya LI-YA katika umoja na wingi.<br>● Mwanafunzi aelezwe kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya LI-YA kwenye sentensi alizosoma.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kushiriki katika mchezo wa kuchopoa kadi za sentensi zenye nomino za ngeli ya LI-YA kutoka kwenye kikapu au boksi na kisha kuzisoma, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchagua sentensi zenye nomino za ngeli ya LI-YA kutoka kwenye orodha ya sentensi na kisha kuzisoma.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya LI-YA kwenye kadi, mti maneno, tarakilishi au kapu maneno, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya LI-YA kwenye kadi za breli, orodha maneno au tarakilishi | Ni vipi unaweza kutambua na kutumia nomino katika ngeli ya LI-YA? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi katika sentensi kwa kutumia viambishi vya umoja na wingi wa nomino katika ngeli ya LI-YA.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuunda sentensi sahihi daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali akitumia nomino za ngeli ya LI-YA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi, Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuunda sentensi sahihi kwenye karatasi za breli au kwenye kifaa cha kidijitali akitumia nomino za ngeli ya LI-YA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi.<br>● Mwanafunzi awasomee au kuwasambazia wenzake na mwalimu sentensi alizozitunga ili kuzitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga mafungu ya maneno.
- Kufikiri kwa kina: mwanafunzi anapowaza kwa kina kuhusu atakachoandika.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kutambua nomino na katika kusikiliza mafungu kwenye tepurekoda.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za vikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza kipakatalishi anachotumia.
- Uzalendo: mwanfunzi anapofanya kazi na wengine kwenye vikundi bila ubaguzi wa kijamii.
- Umoja: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kutoka jamii mbalimbali ili kutekeleza kazi ya kikundi.

**Masuala Mtambuko:**
Umoja na wenzake: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kuandika nomino za ngeli ya LI-YA.
Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapozin gatia hatua za kiusalama anapotumia kifaa cha kidijitali kuandika insha ya wasifu.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili hushughulikia suala la ngeli za nomino.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, kapu maneno, orodha maneno, kadi maneno, kadi za breli, karatasi za breli

## 7.0 MATUNDA NA MIMEA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Nahau**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nahau za maadili na uraia katika matini mbalimbali,<br>b) kutambua maana za nahau mbalimbali za maadili na uraia katika mazungumzo,<br>c) kutumia nahau za maadili na uraia katika mawasiliano,<br>d) kuthamini matumizi ya nahau za maadili na uraia katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nahau za maadili na uraia (k.v. *fanya haki*, *omba kibali*, *omba ruhusa*, *piga hodi* na *taka idhini*) katika chati, michoro, picha, kapu maneno, mti maneno, na katika vyombo vya kidijitali venye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nahau za maadili na uraia kutoka kwa orodha maneno au mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashiriki katika kujadili na wenzake maana za nahau za maadili na uraia.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia nahau za maadili na uraia kutunga sentensi akiwa pekee au kwa kushirikiana na wenzake. | 1. Je unatambua vipi nahau ambazo zinahusu uraia?<br><br>2. Kwa nini ni muhimu kuteua nahau za maadili na uraia kutoka kwenye kundi la nahau? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atazame vibonzo vikijibizana kuhusu nahau na maana zake, mwanafunzi asiyeona asikilize vibonzo vikijibizana kuhusu nahau na maana zake.<br>• Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kuteua nahau za maadili na uraia kutoka kwenye kundi la nahau. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili maana za nahau za maadili na uraia akiwa na wenzake.
- Ujuzi wa kidijital: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kutambua nahau za maadili na uraia.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafuta maana za nahau na kuzitumia kwa ufasaha katika mawasiliano.
- Uraia: mwanafunzi anaposhiriki kujadili masuala ya uraia na yanayolenga suala lengwa.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuteua nahau za maadili na uraia kwa kuonyesha upendo.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi anavyotumia katika kutambua nahau za maadili na za uraia.
- Heshima:wanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanikisha kazi ya kikundi na kuheshimu maoni yao.

**Masuala Mtambuko:**
Umoja wa kijamii: mwanafunzi anaposhiriki katika majadiliano kwa vikundi wanapotunga sentensi kwa kutumia nahau za maadili na uraia.

| |
|---|
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: nahau hufundishwa katika somo hili. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>chati,kapu maneno, orodha maneno, kadi maneno, kadi za breli, michoro, mti maneno,kinasasauti, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.2 Kusoma** | **7.2.1 Kusoma kwa Mapana**<br>● Matini<br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matini ya aina mbalimbali ya kusoma na kuchagua yanayomvutia,<br>b) kusoma matini aliyochagua ili kufaidi ujumbe na lugha iliyotumiwa,<br>c) kufurahia usomaji wa aina mbalimbali za matini. | ● wanafunzi aelekezwe kutambua matini (k.v. *vitabu, majarida, magazeti*) yanayomvutia maktabani na mtandaoni.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma matini aliyochagua ili kufaidi ujumbe na lugha iliyotumiwa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuwasimulia wenzake kuhusu matini aliyosoma ili kupashana ujumbe na kuchocheana kusoma zaidi kwa ajili ya kujifurahisha. | 1. Kwa nini unapenda kusoma?<br>2. Unawezaje kuvutiwa unaposoma hadithi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi ajadiliane na wenzake matini ambayo wamesoma. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposimulia wenzake kuhusu matini aliyoisoma ili kupasha ujumbe na kuchocheana kusoma zaidi kwa ajili ya kujifurahisha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi na mtandao kupata matini ya kusoma.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojichagulia matini na kuyasoma.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anaposimulia wenzake kuhusu matini aliyosoma na kupasha ujumbe uliotumiwa.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza tarakilishi yenye teknolojia saidizi anayoitumia katika kutambua matini.
- Heshima: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu alichokisoma na kusikiliza maoni ya kila mmoja wao.

**Masuala Mtambuko:**
Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anapotambua na kusoma matini yanayomvutia maktabani akizingatia suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili pia hushughulikia kusoma kwa mapana.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

gazeti, jarida, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vitabu

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1 Insha ya Maelezo**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya maelezo katika matini,<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kufuata kanuni zifaazo,<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wa insha ya maelezo ili kukuza ubunifu. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vifungu vya maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kujadili mada na muundo wa insha ya maelezo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandaa vidokezo vitakavyomwongoza kuandika insha yake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya maelezo akizingatia mada lengwa (k.v. *upanzi wa miti na mimea, utunzaji wa mimea, shamba la matunda* n.k.) hasa akizingatia vivumishi na vielezi vifaavyo kutoa picha dhahiri kuhusu anachokielezea.<br>● Mwanafunzi aandike insha ya maelezo akizingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu inayojumuisha methali na nahau alizojifunza awali. | 1. Unawezaje kutambua insha ya maelezo katika matini?<br>2. Je, ni kwa nini unapaswa kufuata kanuni zifaazo unapoandika insha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aandike insha ya maelezo mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili waisome na kuitathmini.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika ili waisikilize na kuitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mjadala ya kujadili mada na muundo wa insha ya maelezo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya maelezo.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo akizingatia suala lengwa.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoyatafakari Swali Dadisi Lililopendekezwa na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi

**Maadili:**
Heshima: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili mada na muundo wa insha ya maelezo.
Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika insha na kuwasambazia wenzake waitathmini.

**Masuala Mtambuko:**
Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo akizingatia mada lengwa (matunda na mimea).

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili hushughulikia uandishi wa insha ya maelezo.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Kielelezo cha insha ya maelezo, vifaa vya breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1**<br><br>**Ngeli ya KI-VI**<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya KI-VI,<br>b) kutambua nomino katika ngeli ya KI-VI ili kuzitofautisha na nomino katika ngeli nyingine,<br>c) kutumia nomino za ngeli ya KI-VI katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi,<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya KI-VI katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kusoma sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya KI-VI katika umoja na wingi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya KI-VI kwenye sentensi alizosoma.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kushiriki katika mchezo wa kuchopoa kadi za sentensi zenye nomino za ngeli ya KI-VI kutoka kwenye kikapu au boksi na kisha kuzisoma, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchagua sentensi zenye nomino za ngeli ya KI- VI kutoka kwenye orodha ya sentensi na kisha kuzisoma.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya KI-VI (k.m. *kitabu*, *kikombe*, *kisu*, *chakula*, *choo*) kwenye kadi, mti maneno, tarakilishi au kapu maneno, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya KI-VI (k.m. *kitabu*, *kikombe*, *kisu*, *chakula*, *choo*) kwenye kadi za breli, orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi. | Ni vipi unaweza kutambua na kutumia nomino katika ngeli ya KI-VI?? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi katika sentensi kwa kutumia viambishi vya umoja na wingi wa nomino katika ngeli ya KI-VI.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuunda sentensi sahihi daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali akitumia nomino za ngeli ya KI-VI katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuunda sentensi sahihi kwenye karatasi za breli au kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akitumia nomino za ngeli ya KI-VI katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi.<br>● Mwanafunzi awasomee au kuwasambazia wenzake na mwalimu sentensi alizozitunga ili kuzitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotaja nomino za ngeli ya KI-VI katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake katika vikundi.
- Ubunifu: mwanafunzi anaposhiriki katika kutunga sentensi akitumia nomino za ngeli ya KI-VI katika umoja na wingi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi kusoma sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya KI-VI katika umoja na wingi.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia na kutunza tarakilishi anaposoma sentensi zilizotungwa kutokana na nomino za KI-VI.
- Heshima: mwanafunzi anapotaja nomino za ngeli ya KI-VIkatika umoja na wingi akishirikiana na wenzake kwa vikundi.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English na Indigenous Languages: masomo haya hushughulikia sarufi . |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Vitabu, vitabu vya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, kadi za sentensi, matini za breli, kadi maneno,mti maneno,kadi za breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.2 Ngeli ya LI-LI**<br><br>(Kipindi 1) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya LI-LI,<br>b) kutambua nomino katika ngeli ya LI-LI ili kuzitofautisha na nomino katika ngeli nyingine,<br>c) kuunda sentensi akitumia nomino za ngeli ya LI-LI, katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi, | ● Mwanafunzi aelekezwe kusoma sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya LI-LI katika umoja na wingi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya LI-LI kwenye sentensi alizosoma.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kushiriki katika mchezo wa kuchopoa kadi za sentensi zenye nomino za ngeli ya LI-LI kutoka kwenye kikapu au boksi na kisha kuzisoma, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchagua sentensi zenye | Ni vipi unaweza kutambua viambishi vya upatanisho? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya LI-LI katika mawasiliano. | nomino za ngeli ya LI-LI kutoka kwenye orodha ya sentensi na kisha kuzisoma.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya LI-LI (k.m. *jua- jua*, *giza-giza*) kwenye kadi, mti maneno, tarakilishi au kapu maneno, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino katika ngeli ya LI-LI (k.m. *jua- jua*, *giza-giza*) kwenye kadi za breli, orodha maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika nomino za ngeli ya LI-LI katika umoja na wingi,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi katika sentensi kwa kutumia viambishi vya umoja na wingi wa nomino katika ngeli ya LI-LI,<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuunda sentensi sahihi daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali akitumia nomino za ngeli ya LI-LI katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuunda sentensi sahihi kwenye karatasi za breli au kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akitumia nomino za ngeli ya LI-LI katika umoja na wingi | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | akizingatia upatanisho wa kisarufi.<br>● Mwanafunzi awasomee au kuwasambazia wenzake na mwalimu sentensi alizozitunga ili kuzitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga mafungu ya maneno kutokana na ngeli ya LI-LI katika umoja na wingi.
- Kufikiri kwa kina: mwanafunzi anapowaza kwa kina kuhusu atakachoandika.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi kutambua nomino na katika kusikiliza mafungu ya maneno yakisomwa.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza kipakatalishi anachokitumia.
- Uzalendo: mwanafunzi anapofanya kazi na wengine kwenye vikundi.

**Masuala Mtambuko:**
Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anapoandika nomino za ngeli ya LI-LI katika umoja na wingi na wenzake bila ubaguzi.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: ngeli za nomino hufundishwa katika somo hili.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

orodha maneno, mti maneno, kapu maneno, tarakilishi yenye teknolojia saidizi , kadi maneno, kadi za breli

## 8.0 WANYAMA WA PORINI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **8.1.1 Visawe**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kisawe ili kukibainisha,<br>b) kutambua maneno mawili yenye maana sawa katika matini,<br>c) kutumia visawe ifaavyo katika mawasiliano,<br>d) kuthamini matumizi ya visawe katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aeleze maana ya neno kisawe akiwa peke yake au kwa kujadiliana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua maneno mawili ya kiwango chake yenye maana sawa (*k.v. tembo – ndovu, kinyonga – lumbwi, adui-hasimu, siri-faragha, baba-abu, barua-waraka, ami- amu, televisheni-runinga)* kwa kurejelea kapu maneno, kadi za maneno na mti maneno, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua maneno mawili ya kiwango chake kutoka kwenye orodha maneno.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuambatanisha visawe katika kapu maneno, mti maneno, ubao, chati, vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, kadi za maneno. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuambatanisha visawe kutoka kwenye orodha maneno na tarakilishi yenye teknolojia saidizi. | Ni kwa nini tunapaswa kutumia visawe ifaavyo katika mawasiliano? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona ahusishe visawe na vifaa halisi, picha, michoro kwenye chati, kitabu au katika vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuhusisha visawe na vifaa halisi kwenye mazingira, maelezo ya michoro, kitabu au katika vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi ashiriki kujadili visawe mbalimbali katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili au Zaidi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutumia kisawe kimoja kuchukua nafasi ya kingine katika sentensi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wengine kueleza maana na neno kisawe kwa kujadiliana.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapofikiria kuhusu visawe mwafaka na uhusiano wa visawe na vifaa halisi
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kama nyenzo za kufaulisha mada.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake kujadili visawe mbalimbali katika vikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotekeleza majukumu yao katika vikundi a vilevile kutunza vifaa anavyotumia katika somo.

**Masuala Mtambuko:**

Umoja wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili visawe mbalimbali darasani.

| |
|---|
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili hushirikisha mada ya visawe. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Mti maneno, kapu maneno, orodha maneno, ubao, kapu maneno, maelezo ya michoro, michoro. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>*Mchezo mfupi wa kuigiza*<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya mchezo wa kuigiza, mhusika na maelekezo,<br>b) kutambua mchezo wa kuigiza katika matini,<br>c) kutambua wahusika na maelekezo katika mchezo mfupi wa kuigiza,<br>d) kusoma mchezo mfupi wa kuigiza kwa ufasaha kwa kuzingatia ujumbe, | ● Mwanafunzi ashiriki katika majadiliano kuhusu maana za mchezo wa kuigiza, mhusika na maelekezo akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua mchezo wa kuigiza, wahusika na maelekezo katika matini mbalimbali kama vile vitabu, chati na vilevile kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atazame mchezo mfupi wa kuigiza ukiigizwa darasani au kwenye vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona apewe maelezo ya maigizo darasani au kwenye vifaa | Ni vipi unaweza kutambua mchezo wa kuigiza katika matini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e) kufurahia kusoma michezo na kuiigiza. | vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma mchezo wa kuigiza akizingatia maelekezo na ujumbe.<br>● Mwanafunzi ashiriki mjadala kuhusu ujumbe unaojitokeza kwenye mchezo wa kuigiza.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma mchezo wa kuigiza kwenye mtandao.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujibu maswali yanayotokana na mchezo wa kuigiza aliosoma. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika majadiliano kuhusu maana za mchezo wa kuigiza na wenzake.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotazama au kusikiliza mchezo mfupi wa kuigiza kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.
- Uwazaji wa kina: mwanafunzi anapong'amua ujumbe uliomo kwenye mchezo.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposhiriki katika kusoma na kushiriki mjadala kuhusu ujumbe unaojitokeza kwenye mchezo wa kuigiza.

**Maadili:**
Heshima: mwanafunzi anaposhiriki katika majadiliano kuhusu maana ya mchezo wa kuigiza akiwa na wenzake na kuthamini mchango wao.

| **Masuala Mtambuko:**<br>Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu utunzaji wa wanyama wa porini na elimu ya mazingira. |
|---|
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia michezo ya kuigiza. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vitabu vyenye matini za breli, vitabu vilivyoidhinishwa |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.3 Kuandika** | **8.3.1 Insha ya Masimulizi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya masimulizi kwa kuzingatia muundo,<br>b) kuandika insha ya masimulizi kwa kufuata kanuni zifaazo,<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wa insha ya masimulizi ili kujenga ubunifu wake. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua insha ya masimulizi kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandaa vidokezo vitakavyomwongoza kuandika insha yake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha inayosimulia kisa cha tukio linalohusiana na wanyama wa porini kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati | Ni vipi unaweza kuandika insha ya masimulizi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu.<br>● Mwanafunzi ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya masimulizi.<br>● Mwanafunzi aandike insha ya masimulizi mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili waisome na kuitathmini.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika ili waisikilize na kuitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili mada ya insha na muundo wa insha ya masimulizi na wenzake.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya masimulizi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapobuni na kuandika insha ya masimulizi.

**Maadili:**
Upendo: mwanafunzi anapojitolea kuisambaza insha aliyoiandika mtandaoni kwa wenzake na mwalimu ili waisome na waitathmini.
Uwajibikaji: mwanafunzi anapoandika insha inayosimulia kisa cha tukio linalohusiana na wanyama wa porini kwa kuzingatia mpangilio ufaao.

| Masuala Mtambuko: |
|---|
| Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapoandika insha inayosimulia kisa cha tukio linalohusiana na wanyama wa porini.<br>Elimu ya fedha: mwanafunzi anapotunga sentensi akizingatia umuhimu wa wanyama pori. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia uandishi wa insha ya masimulizi. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kielelezo cha insha ya masimulizi, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.4 Sarufi** | **8.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi**<br>● *Kauli ya kutenda*<br>● *Kauli ya Kutendea*<br>● *Kauli ya kutendwa*<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya mnyambuliko wa vitenzi ili kuubainisha,<br>b) kueleza maana ya kauli za kutenda, kutendea na kutendwa ili kuzitofautisha,<br>c) kutambua vitenzi katika kauli za kutenda, kutendea na kutendwa katika matini,<br>d) kutumia vitenzi katika kauli za kutenda, kutendea na | ● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kueleza maana za mnyambuliko wa vitenzi, kauli ya kutenda, kauli ya kutendea na kauli ya kutendwa.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vitenzi katika kauli za kutenda, kutendea na kutendwa katika chati, jedwali, kapu maneno, mti maneno, ubao na vyombo vya kidijitali vya teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua vitenzi | Ni vipi vitenzi vinaweza kubadilika mwishoni ili kuleta maana mbalimbali? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kutendwa ipasavyo anapowasiliana,<br>e) kuchangamkia matumizi ya vitenzi katika kauli za kutenda, kutendea na kutendwa kwenye mawasiliano. | katika kauli za kutenda, kutendea na kutenda katika orodha maneno na vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kunyambua vitenzi katika kauli lengwa akiwa peke yake, wakiwa wawili wawili au katika vikundi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia vitenzi katika kauli lengwa kwenye sentensi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona ashirikiane na wenzake kujaza nafasi katika jedwali la mnyambuliko wa vitenzi kwenye daftari au kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika mnyambuliko wa vitenzi kwenye karatasi za breli au kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika sentensi upya kwa | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kueleza maana ya mnyambuliko wa vitenzi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anaponyambua vitenzi katika kauli mbalimbali.
- Kujiamini:mwanafunzi anapotoa majibu na kuandika sentensi upya kwa kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali.

**Masuala Mtambuko:**
Umoja wa kijamii: mwanafunzi anaponyambua vitenzi katika kauli lengwa akiwa na wenzake.
Elimu ya utunzaji wanyama: mwanafunzi anyambue vitenzi vya kauli lengwa kwa sentensi akizingatia mada lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili pia hushughulikia vitenzi.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Mti maneno, orodha maneno, ubao, chati,tarakilishi yenye teknolojia saidizi na chati, vifaa vya breli

## 9.0 AFYA BORA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Mazungumzo ya Kimuktadha**<br><br>*Miktadha isiyo rasmi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua miktadha ya mawasiliano isiyo rasmi,<br>b) kutumia lugha kuhusiana ipasavyo katika miktadha isiyo rasmi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya lugha katika miktadha isiyo rasmi. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua mazungumzo yasiyo rasmi kwa kutazama maigizo ya mazungumzo lengwa kwenye video na tarakilishi yenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona asikilize maelezo ya maigizo kwenye video na tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kuigiza mazungumzo katika miktadha isiyo rasmi (k.m. *akicheza na wenzake, akizungumza na wazazi, ndugu, nyanya au babu nyumbani*).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua umuhimu wa nidhamu ya lugha, hata katika mazingira yasiyo rasmi (k.m. *kutumia lugha ya upole, heshima na kumpa mwenzake nafasi ya kuzungumza na kusikiliza kwa makini anaposhiriki katika mazungumzo).* | Ni kwa nini tunatumia lugha isiyo rasmi? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td><ul><li>Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kutaja miktadha ya mazungumzo yasiyo rasmi (k.v. wanapocheza, wanapozungumza na marafiki, wakiwa nyumbani, n.k),</li><li>Mwanafunzi asikilize mazungumzo kati ya mtoto na babu au nyanya ama kati ya watoto pekee yaliyorekodiwa kwa kutumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.</li></ul></td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<ul><li>Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutaja miktadha ya mazungumzo yasiyo rasmi.</li><li>Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposikiliza mazungumzo yaliyorekodiwa kwa kutumia kifaa cha kidijitali ili kukuza msamiati wa lugha.</li><li>Ubunifu: Mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuigiza mazungumzo katika miktadha mbalimbali</li><li>Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza au kutazama mazungumzo.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>Haki za kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake wa jamii mbalimbali na kuheshimu mchango wao katika mazungumzo yasiyo rasmi.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala Mtambuko:<br>Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuigiza mazungumzo yanayolenga maswala makuu ya lishe bora na mazingira.</td></tr>
</table>

| |
|---|
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia mazungumzo katika miktadha mbalimbali. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Nyenzo halisi, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, kinasasauti. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.2 Kusoma** | **9.2.1 Kusoma kwa Mapana**<br><br>*Matini ya kujichagulia*<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matini ya kusoma ya aina mbalimbali na kuchagua yanayomvutia,<br>b) kusoma matini alizochagua ili kufaidi ujumbe na lugha iliyotumiwa,<br>c) kufurahia usomaji wa aina mbalimbali za matini ili kupanua mawazo yake. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua matini (k.v. *vitabu, majarida, magazeti*) zinazovutia maktabani na mtandaoni.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma matini aliyochagua (yakijumuisha yale yenye mada ya afya bora) ili kufaidi ujumbe na lugha iliyotumiwa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuwasimulia wenzake kuhusu matini aliyosoma ili kupashana ujumbe na kuchocheana kusoma zaidi kwa ajili ya kujifurahisha.<br>● Mwanafunzi ajadiliane na wenzake matini ambayo wamesoma. | Kwa nini unapenda kusoma? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposimulia na kujadiliana na wenzake matini aliyoisoma ili kupashana ujumbe na kuchocheana kusoma zaidi kwa ajili ya kujifurahisha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kupata matini ya kusoma.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojichagulia matini na kusoma kwa mapana.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza matini anayosoma pamoja na nyenzo zingine.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuhusu matini aliyosoma ili kujifurahisha na kupanua mawazo yake.

**Masuala Mtambuko:**
Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anaposoma matini yanayojumuisha mada ya afya bora ili kufaidi ujumbe uliotumiwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili linashughulikia kusoma kwa mapana.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Majarida, vitabu vya breli,vitabu vilivyoidhinishwa, magazeti, tarakilishi yenye teknolojia saidizi

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.3 Kuandika** | **9.3.1 Insha ya Maelezo**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya maelezo katika matini,<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kufuata kanuni zifaazo,<br>c) kuchangamkia utunzi wa insha ya maelezo ili kujenga ubunifu wake. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vifungu vya maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandaa vidokezo vitakavyomwongoza kuandika insha yake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya maelezo akitumia lugha ifaayo kutoa picha dhahiri kuhusu anachokieleza.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya maelezo akizingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na lugha ya kiubunifu inayojumuisha methali na nahau alizojifunza awali.<br>● Mwanafunzi ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha (*ihusiane na mada ya afya bora*) na muundo wa insha ya maelezo. | Ni kwa nini tunapaswa kuzingatia mambo muhimu tunapoandika insha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | <ul><li>Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya maelezo mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili waisome na kuitathmini.</li><li>Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika ili waisikilize na kuitathmini.</li></ul> | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowasambazia wenzake insha ya maelezo aliyoiandika ili waisome na kuithamini.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya maelezo.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo matandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili waisome na kuithamini.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoyatafakari maswali dadisi na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi.

**Maadili:**
Heshima: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu mada ya insha inayohusu afya bora na muundo wake katika kikundi.
Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kufanikisha kazi yake na kusambazia wenzake mtandaoni.

**Masuala Mtambuko:**
Umoja wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka maeneo mbalimbali katika shughuli za kikundi.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili linafunza uandishi wa insha ya maelezo.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**
picha, maelezo ya picha, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli,

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1 Vinyume vya Nomino**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kinyume cha nomino ili kukibainisha,<br>b) kutambua vinyume vya nomino katika matini,<br>c) kutumia vinyume vya nomino ipasavyo katika matini,<br>d) kuchangamkia matumizi ya vinyume vya nomino katika mawasiliano ya kila siku. | • Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya kinyume cha nomino akishirikiana na wenzake.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vinyume vya nomino (k.v. *rafiki – adui*, *mgeni – mwenyeji*, *furaha – huzuni*, *uhuru-utumwa*, *mfalme- malkia*, *usiku – mchana*, *tajiri – maskini*, n.k) katika chati, kadi za maneno, kapu maneno, mti maneno au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua vinyume vya nomino katika orodha maneno na tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kutafuta vinyume vya nomino kwa kurejelea orodha ya nomino alizopewa.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutalii mazingira yake na kuunda orodha ya vinyume vya nomino za vitu halisi anavyoweza kutambua.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kwa kutumia vinyume vya | Ni vipi unaweza kutumia vinyume vya nomino ipasavyo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | nomino kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake darasani kutafuta vinyume vya nomino.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi kwa kutumia vinyume vya nomino ipasavyo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa vya kidijitali chenye teknolojia saidizi kutambua vinyume vya nomino.
- Uwazaji wa kina na utatuzzi wa matatizo: mwanafunzi anapotafuta vinyume vya nomino akirejelea orodha aliyopea ipasavyo.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza kifaa cha kidijitali na nyenzo zingine anazotumia katika kufanikisha kazi yake.
- Heshima: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kikundi na kuthamini maoni yao.

**Masuala Mtambuko:**
Elimu ya mazingira: mwanafunzi anapotalii mazingira yake na kuunda orodha ya vinyume anavyoweza kutambua.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili linashughulikia vinyume vya nomino.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Orodha maneno, kadi maneno, kadi za breli,kapu maneno, mti maneno na tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli

## 10.0 KUKABILIANA NA UHALIFU

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.1 Kusikiliza na kuzungumza** | **10.1.1 Tashbihi:**<br>● *Tashbihi za kimo*<br>● *Tashbihi za umbo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya tashbihi ili kuibainisha,<br>b) kutambua tashbihi za kimo na umbo katika matini,<br>c) kutumia tashbihi za kimo na umbo kwa usahihi katika sentensi,<br>d) kufurahia matumizi ya tashbihi za kimo na umbo katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kuelezea maana ya tashbihi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua tashbihi za kimo na umbo (k.v. *mrefu kama twiga, mfupi kama nyundo, mwembamba kama sindano, konda kama ng'onda)* katika vitabu, chati na vyombo vya kidijitalivyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kurejelea picha au michoro kwenye chati au tarakilishi teknolojia saidizi ili kutumia tashbihi zifaazo kutolea maelezo, mwanafunzi asiyeona apewe maelezo ya picha au michoro kwenye chati au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi akitumia tashbihi za kimo na umbo akiwa peke yake au katika vikundi. | Unatofautisha vipi tashbihi za kimo na umbo katika matinii? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aelekezwe kukamilisha sentensi zinazolinganisha vitu viwili kwa kutumia tashbihi za kimo na Umbo.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuwasilisha sentensi zake darasani ili wenzake wazitolee maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kazi ya vikundi kueleza maana ya tashbihi za kimo na umbo.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojaribu kukamilisha kazi ya ziada anayopewa kuhusu tashbihi za kimo na umbo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kujifunza tashbihi za kimo na umbo.

**Maadili:**
Heshima: mwanafunzi anapotangamana na wenzake na kuelezea maana za tashbihi mbalimbali.
Uwajibikaji: Mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kutunga sentensi.

**Masuala Mtambuko:**
Elimu ya mazingira: mwanafunzi anarejelea mifano ya vitu na viumbe katika mazingira yake.
Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka maeneo mbalimbali kuelezea maana ya tashbihi za umbo na kimo.

**Uhusiano na masomo mengine:**
English: somo hili linashughulikia suala la tashbihi.

**Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**

Orodha maneno, michoro, maelezo ya picha au michoro, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kusoma** | **10.2 Kusoma Matini ya kidijitali**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua na kuzingatia hatua za kiusalama katika matumizi ya vifaa vya kidijitali,<br>b) kutambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma ili kuimarisha umilisi wake wa kutumia tarakilishi,<br>c) kusakura matini kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma vyenye mada lengwa,<br>d) kusoma matini lengwa ili kupata ujumbe,<br>e) kuchangamkia matumizi ya vifaa vya kidijitali katika kutafuta na kusoma ujumbe ili kuimarisha maarifa yake. | ● Mwanafunzi aliye upungufu wa kuona aelekezwe kutambua na kuzingatia hatua za kiusalama kutoka kwenye chati au kwenye tarakilishi na mitandao, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua na kuzingatia hatua za kiusalama kutoka kwenye orodha aliyopewa au kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi na mitandao.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua jina la faili lengwa kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi na kufanya mazoezi ya kuifungua na kuifunga.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua mitandao salama yenye matini yanayoafiki kiwango na mahitaji yake.<br>● Mwanafunzi atambue umuhimu wa kutoa habari kwa mwalimu, mzazi au mlezi wake endapo atapata ujumbe kutoka kwa watu asiowajua mtandaoni na kutowasiliana nao. | Tunatumia vipi vifaa vya kidijitali tunaposoma matini? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>● Mwanafunzi aelekezwe kutafuta maana za maneno mapya kwenye kamusi mtandaoni.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma matini kwenye tovuti salama.<br>● Mwanafunzi asikilize matamshi na maelezo kuhusu anachokisoma mtandaoni panapowezekana.<br>● Mwanafunzi atoe habari kuhusu matini aliyosoma kwa muhtasari na kujibu maswali katika maandishi au mazungumzo na wenzake.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi katika kutafuta, kusakura na kusoma matini.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapopata hamu ya kutafuta matini ya kusoma kwenye tarakilishi na mitandaoni.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapoutunza kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kuzingatia mitandao salama.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kutoa habari kwa muhtasari kuhusu matini aliyoisoma ili waiboreshe.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala Mtambuko:<br>● Usalama wa mtandaoni: mwanafunzi anapozingatia hatua za kiusalama anaposakura matini kwenye tovuti.<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka jamii tofauti tofauti kufanya shughuli ya kikundi.</td></tr>
</table>

| |
|---|
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Masomo yote yanazingatia matumizi ya vifaa vya kidijitali ili kukuza ujuzi wa kidijitali. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, chati, kamusi mbalimbali |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1 Insha ya Masimulizi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya masimulizi kwa kuzingatia ujumbe, mtindo na muundo,<br>b) kuandika insha ya masimulizi kwa kufuata kanuni zifaazo,<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wa insha ya masumulizi ili kujenga ubunifu wake. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua insha ya masimulizi kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandaa vidokezo vitakavyomwongoza kuandika insha yake.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya masimulizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika insha inayosimulia kisa cha tukio linalohusiana na uhalifu wa kawaida daftarini kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati | Je, unajiandaa vipi ili kuandika insha nzuri ya masimulizi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika insha inayosimulia kisa cha tukio linalohusiana na uhalifu wa kawaida kwenye karatasi za breli kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, nukta nundu zifaazo, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya masimulizi mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili waisome na kuitathmini.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika ili waitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi ya kikundi kujadili mada na muundo wa insha ya masimulizi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika insha mtandaoni kwa kurejelea kielelezo cha insha ya masimulizi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya masimulizi kwa kufuata kanuni zifaazo.

| **Maadili:** |
|---|
| ● Heshima: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadilli mada na muundo wa insha ya masimulizi na kuthamini mchango wao.<br>● Amani: mwanafunzi anapojitolea kuwasomea wenzake insha aliyoandika kwa upendo. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Kukabiliana na uhalifu: mwanafunzi anapoandika kisa cha tukio linalohusiana na uhalifu wa kawaida.<br>● Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili mada na muundo wa insha ya masimulizi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia uandishi wa insha ya masimulizi. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kielelezo cha insha ya masimulizi, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Nyakati na hali**<br>● *Wakati uliopita*<br>● *Wakati uliopo*<br>● *Wakati* | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya wakati uliopita, uliopo na ujao kwenye vitenzi,<br>b) kutambua vitenzi katika wakati | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua viambishi vinavyobainisha nyakati mbalimbali (*uliopita, uliopo na ujao*) kwenye sentensi zilizoonyeshwa kwenye chati, ubao au kwa kutumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi k.v. tarakilishi na projekta, | Unatofautisha vipi viambishi kulingana na wakati? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | *ujao*<br><br>(Vipindi 3) | uliopita, uliopo na ujao kwenye matini,<br>c) kutunga sentensi akitumia vitenzi katika wakati uliopita, uliopo na ujao,<br>d) kufurahia zoezi la kutunga sentensi akiwa na wenzake. | mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua viambishi vinavyobainisha nyakati mbalimbali (*uliopita*, *uliopo na ujao*) kwenye sentensi zilizoonyeshwa kwenye orodha sentensi au kwa kutumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi k.v. tarakilishi na projekta.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutunga sentensi akitumia vitenzi katika nyakati mbalimbali hali ya kuendelea katika mazungumzo, kuandika daftarini au kupiga chapa kwenye tarakilishi/ kipakatalishi chenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutunga sentensi akitumia vitenzi katika nyakati mbalimbali hali ya kuendelea katika mazungumzo, kuandika kwenye karatasi za breli au kupiga chapa kwenye tarakilishi/ kipakatalishi chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake katika vikundi kutaja sentensi katika wakati fulani na kuzibadilisha katika wakati tofauti hali ya kuendelea, | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi atunge sentensi katika nyakati mbalimbali hali ya kuendelea kwenye blogi ili wenzake waweze kuzisoma na kuzitathmini,<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika upya sentensi katika wakati mmoja hali ya kuendelea ziwe katika nyakati tofauti hali ya kuendelea daftarini, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika upya sentensi katika wakati mmoja hali ya kuendelea ziwe katika nyakati tofauti hali ya kuendelea kwenye karatasi za breli.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi kwenye sentensi kwa kutumia vitenzi katika nyakati mbalimbali hali ya kuendelea. | |

- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofaulu kutunga sentensi sahihi katika nyakati mbalimbali hali ya kuendelea.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kipakatalishi au tarakilishi kutunga sentensi na vilevile kuzisambaza mtandaoni.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapojifunza kuthamini maoni ya wenzake katika shughuli ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na nyenzo zingine kufanikisha kufanikisha kazi yake.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kubainisha nyakati mbalimbali.<br>● Kupambana na ufundishaji wa misimamo mikali: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia dhana ya nyakati na hali. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Tarakilishi yenye teknolojia saidizi, projekta, vifaa vya breli, chati, karatasi za breli |

## 11.0 MAPATO

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.1 Kusikiliza na kuzungumza** | **11.1.1 Masimulizi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kusikiliza masimulizi kwa kuzingatia ujumbe,<br>b) kusimulia tungo kwa kuzingatia mada, ubunifu na usanifu wa lugha mbele ya wenzake,<br>c) kutumia ishara zifaazo ili kuimarisha masimulizi yake,<br>d) kuchangamkia masimulizi katika mazingira mbalimbali. | ● Mwanafunzi asikilize masimulizi yanayohusiana na suala lengwa yakitolewa na mgeni mwalikwa, mwalimu, mwanafunzi mwenzake au kutokana na vifaa vya kidijitali.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujibu maswali kutokana na masimulizi aliyosikiliza.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua msamiati wa suala lengwa uliotumiwa katika masimulizi aliyosikiliza.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kubuni simulizi linalohusiana na mada husika kwa kutazama picha, michoro au kujadiliana na wenzake, mwanafunzi asiyeona aelekezwe | Je, tunajiandaa vipi ili kutoa masimulizi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kubuni simulizi linalohusiana na mada husika kwa kusikiliza maelezo ya picha, maelezo ya michoro au kujadiliana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutoa maelezo kuhusu mada lengwa (k.v. *jinsi ya kujipatia riziki, Jinsi ya kutumia mapato yake, n.k.).*<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia ishara za mwili zifaazo k.v ishara za uso, za mikono, mabega kuimarisha masimulizi yake.<br>● Mwanafunzi ajadiliane na wenzake kuhusu ubora wa masimulizi aliyosikiliza. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu ubora wa masimulizi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga simulizi linalohusiana na mada husika kwa kutazama picha au michoro.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposimulia kisa mbele ya wenzake.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>Heshima: mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika mjadala kuhusu ubora wa masimulizi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Elimu ya fedha: mwanafunzi anaposimulia kisa kuhusu ujuzi wa matumizi ya fedha na mapato.<br>Umasikini: mwanafunzi anaposikiliza na kuzungumzia kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia kusikiliza na kuzungumza. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Mgeni mwalikwa, kielelezo cha masimulizi, picha, maelezo ya picha, michoro, maelezo ya michoro,vifaa vya breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.2 Kusoma** | **11.2.1**<br><br>**Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha,<br>b) kusoma kifungu cha hadithi kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu cha hadithi kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti,<br>d) kusoma kifungu cha hadithi kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu cha hadithi kwa kuambatanisha ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusoma makala kwa ufasaha.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu cha hadithi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu cha hadithi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti (k.v. kiwango cha sauti na kiimbo).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu cha hadithi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno yasiyopungua 75 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi) ili wenzake wamtolee maoni.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo panapofaa anaposoma (k.v. ishara za uso na mikono), mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma | Je, kwa nini mapato ni muhimu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kifungu kwa kuambatanisha toni ifaayo anaposoma.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma hadithi kuhusu masuala mtambuko mbalimbali kutoka kwenye vitabu, vifaa vya kidijtali vyenye teknolojia saidizi, n.k akizingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kiwango kifaacho cha sauti. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi kujadili umuhimu wa mapato.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi katika kutazama au kusikiliza vibonzo kwenye video na tarakilishi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafuta hadithi mbalimbali na kuzisoma kwa kuzingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kiwango kifaacho cha sauti.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kusoma kifungu cha hadithi kwa kuzingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kiwango kifaacho cha sauti.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma kifungu cha hadithi.
- Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali.

**Masuala Mtambuko:**
Elimu ya fedha: mwanafunzi anaposhiriki katika mjadala wa umuhimu wa mapato pamoja na wenzake.
Umasikini**:** mwanafunzi anaposhiriki katika mjadala kuhusu jinsi ya kupigana na umasikini.

| |
|---|
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili pia linashughulikia kusoma kwa ufasaha. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Tarakilishi yenye teknolojia saidizi, projekta, kadi za maneno, kadi za breli, chati, mti maneno, orodha maneno |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.3 Kuandika** | **11.3.1 Barua ya Kirafiki**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua barua ya kirafiki kwa kuzingatia muundo,<br>b) kuandika barua ya kirafiki kwa kuzingatia ujumbe, mtindo na muundo ufaao,<br>c) kuchangamkia umuhimu wa barua katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua barua ya kirafiki kwa kurejelea vielelezo vya barua za kirafiki zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi yenye teknolojia saidizi,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandaa vidokezo vitakavyomwongoza kuandika insha yake<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kujadili mada ya barua ya kirafiki na vipengele vyake,<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika barua ya kirafiki daftarini yenye kuzingatia mada ya mapato kwa rafiki, ndugu, mzazi n.k. kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, | Ni kwa nini tunaandika barua za kirafiki? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika barua ya kirafiki kwenye karatasi ya breli yenye kuzingatia mada ya mapato kwa rafiki, ndugu, mzazi n.k. kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika insha ya barua kuhusu kupigana na umasikini,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika barua ya kirafiki mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili waisome na kuitathmini,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuwasomea wenzake barua ya kirafiki aliyoandika ili waitathmini,,<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake katika vikundi kujadili kuhusu umuhimu wa barua za kirafiki katika mawasiliano. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi ya kikundi kujadili mada ya barua ya kirafiki na vipengele vyake<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika insha mtandaoni na kurejelea vielelezo vya barua za kirafiki.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoyatafakari swali sadisi lililopendekezwa na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi. |
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhiriki katika mjadala na wenzake na kuthamini maoni yao.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika barua kuhusu kupigana na umasikini. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Ujuzi wa matumizi ya fedha: mwanafunzi anapoandika barua ya kirafiki kuhusu mapato yanayotokana na shughuli mbalimbali.<br>● Utangamano wa kijamii: mwanafunzi an aposhirikiana na wenzake kutoka jamii mbalimbali kujadili mada ya barua ya kirafiki.<br>● Umasikini: mwanafunzi anapoandika kuhusu jinsi ya kupigana na umasikini. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia uandishi wa barua ya kirafiki. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kielelezo cha barua ya kirafiki, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.1 Ukanushaji:**<br>● Wakati uliopita<br>● Wakati uliopo<br>● Wakati ujao<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ukanushaji ili kuubainisha,<br>b) kutambua maneno yaliyokanushwa katika wakati uliopita, uliopo na ujao,<br>c) kutambua viambishi vya nafsi na wakati uliopita, uliopo na ujao katika maneno,<br>d) kukanusha sentensi kwa kuzingatia nafsi na wakati uliopita, uliopo na ujao,<br>e) kuchangamkia ukanushaji wa vitenzi katika mawasiliano | ● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kueleza maana ya ukanushaji<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua maneno yaliyokanushwa kwenye chati, ubao, kapu maneno, mti maneno na vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua maneno yaliyokanushwa kwenye ordha maneno na vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua viambishi vya nafsi na wakati katika maneno akishirikiana na wenzake,<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kukanusha maneno na sentensi akizingatia nafsi na nyakati kwenye daftari au kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kukanusha maneno na sentensi akizingatia nafsi na nyakati kwenye karatasi za breli au kwa kutumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi, | Ni kwa nini tunakunusha maneno? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona asikilize au atazame vipindi vya ukanushaji wa nafsi na wakati kupitia vyombo vya kidijitali, Mwanafunzi asiyeona asikilize vipindi vya ukanushaji wa nafsi na wakati kupitia vyombo vya kidijitali vyenye teknolijia saidizi.<br>• Mwanafunzi aelekzwe kuwasilisha sentensi zake darasani ili wenzake wazitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili mada kwenye vikundi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapojaribu kukanusha maneno na sentensi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kukanusha maneno na sentensi za nafsi na nyakati.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposhiriki katika kazi za kikundi na kuthamini mchango wa wenzake.
- Uadilifu: mwanafunzi anaposikiliza au kutazama vipindi vya ukanushaji katika vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.

**Masuala Mtambuko:**

- Utunzi na usalama wa watoto: mwanafunzi anapokuza uwezo wa kukubali au kukataa mambo mbalimbali kupitia kipindi cha ukanushaji wa nafsi.
- Umasikini: mwanafunzi anapotunga sentensi mbalimbali kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

English: somo hili linashughulikia ukanushaji.

| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia** |
|---|
| Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli, chati, ubao, kapu maneno, kadi za breli, mti maneno,orodha maneno |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.2 Ukubwa wa Nomino**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ukubwa wa nomino ili kuubainisha,<br>b) kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** na zenye mzizi wa silabi moja,<br>c) kutambua nomino katika hali ya ukubwa,<br>d) kubadilisha nomino kutoka hali wastani kuwa katika hali ya ukubwa,<br>e) kutumia nomino katika hali ya ukubwa kwenye sentensi,<br>f) kufurahia kutumia nomino katika hali ya ukubwa kwa usahihi ili kuimarisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** na zenye mzizi wa silabi moja *(k.m mti, mto, mji)* kwenye chati, ubao, mti maneno, kapu maneno au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** na zenye mzizi wa silabi moja *(k.m mti, mto, mji)* kwenye orodha maneno au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashiriki katika vikundi kubadilisha nomino kutoka hali ya wastani hadi hali ya ukubwa.<br>● Mwanafunzi ashiriki katika mchezo wa vikundi: kikundi kimoja kitaje wastani wa nomino na kingine kitaje ukubwa wa nomino hiyo. | Utatambua vipi ukubwa wa nomino? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona, aelekezwe kuburura na kuambatanisha orodha ya nomino katika hali ya ukubwa na orodha nyingine ya nomino katika hali ya wastani kwenye tarakilishi, mwanafunzi asiyeona apewe orodha ya nomino katika hali ya ukubwa na orodha nyingine ya nomino katika hali ya wastani kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi na aelekezwe kuziambatanisha.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi zinazorejelea nomino lengwa katika ukubwa akiwa peke yake au kwenye vikundi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki mijadala kuhusu ukubwa wa nomino.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi kutambua na kuambatanisha nomino katika hali ya wastani na ukubwa.

**Maadili:**
Ushirikiano: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
Haki za kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka jamii mbalimbali katika kutunga sentensi zinazohusu nomino lengwa.

**Masuala Mtambuko:**
Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anapokuza uraia wema kwa kutangamana na wenzake kutoka maeneo tofauti tofauti.
Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kutambua udogo na ukubwa wa nomino.

| |
|---|
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: Somo hili linashughulikia dhana ya ukubwa wa nomino. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Chati, ubao, mti maneno, kadi za breli, orodha maneno, kapu maneno au vifaa vya kidijitali chenye teknolojia saidizi, Vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.3 Udogo wa Nomino**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya udogo wa nomino ili kuubainisha,<br>b) kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** na zenye mzizi wa silabi moja,<br>c) kutambua nomino katika hali ya udogo,<br>d) kubadilisha nomino katika hali wastani kuwa | ● Mwanafaunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** na zenye mzizi wa silabi moja *(k.m mti, mto, mji)* kwenye chati, ubao, mti maneno, kapu maneno au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi, mwanafaunzi asiyeona aelekezwe kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** na zenye mzizi wa silabi moja *(k.m mti, mto, mji)* kutoka kwenye orodha maneno au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashiriki katika vikundi kubadilisha nomino kutoka hali ya wastani hadi hali ya udogo. | Ni vipi unaweza kutambua nomino katika sentensi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | katika hali ya udogo,<br>e) kutumia nomino katika hali ya udogo kwenye sentensi,<br>f) kufurahia kutumia nomino katika hali ya udogo ili kuimarisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi ashiriki katika mchezo wa vikundi: kikundi kimoja kitaje wastani wa nomino na kingine kitaje udogo wa nomino husika.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona apewe orodha ya nomino katika hali ya udogo na orodha nyingine ya nomino katika hali ya wastani kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi ili aziburure na kuziambatanisha, mwanafunzi asiyeona apewe orodha ya nomino katika hali ya udogo na orodha nyingine ya nomino katika hali ya wastani kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi ili kuziambatanisha.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi zinazorejelea nomino lengwa katika udogo akiwa peke yake au kwenye vikundi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kubadilisha nomino kutoka hali ya wastani hadi ya udogo.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi zinazorejelea nomino lengwa katika hali ya wastani na udogo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi vyenye teknolojia saidizi kutambua na kuambatanisha nomino katika hali ya wastani na udogo.

**Maadili:**
Ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya kazi katika kikundi.
Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kikundi kwa heshima.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi zinazorejelea nomino lengwa katika ukubwa na udogo. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English: somo hili linashughulikia dhana ya udogo wa nomino. |
| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Chati, ubao, mti maneno,ordha maneno,kadi za breli, kapu maneno au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

**MWONGOZO WA VIWANGO NA VIGEZO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA**

**MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kuwasiliana kwa kuzingatia matamshi bora** (*Matamshi ya sauti zinazokaribiana: p/b, t/d, k/g, ch/j*) | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti 7 – 8 zilizolengwa kila wakati. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti 5-6 zilizolengwa. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya baadhi ya sauti 3-4 zilizolengwa. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya baadhi ya sauti 1-2 zilizolengwa. |
| **Kuweza kuzungumza na kujieleza kwa ufasaha** *(Kwa kutumia maneno ya upole(kwenda msalani, kwenda haja kubwa, kwenda haja ndogo, kuendesha, makalio, sehemu za siri* na *kujifungua*) *na mazungumzo ya kimuktadha)* | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha na kikamilifu akitumia maneno 6-7 ya upole na katika miktadha mbalimbali. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akitumia maneno ya upole 4-5 na katika miktadha mbalimbali. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akitumia maneno 2-3 ya upole na katika miktadha mbalimbali. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akitumia neno 1 la upole. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kusikiliza na kujibu ipasavyo** **(***Maamkuzi na maagano, ushairi, masimulizi*) | Anasikiliza na kujibu maamkuzi na maagano, kusikiliza na kutoa masimulizi, na kukariri mashairi kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo kwa ubunifu. | Anasikiliza na kujibu maamkuzi na maagano, kusikiliza na kutoa masimulizi na kukariri mashairi kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo. | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi na maagano, kusikiliza na kutoa masimulizi, na kukariri mashairi kwa kiasi kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo. | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi na maagano, kusikiliza na kutoa baadhi ya masimulizi, na kukariri baadhi ya mashairi kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutumia lugha kiubunifu** *(Vitendawili, methali nahau, visawe, tashbihi)* | Anazungumza kwa kuzingatia vipengele 5 vya lugha ya kiubunifu. | Anazungumza kwa kuzingatia vipengele 4 vya lugha ya kiubunifu. | Anazungumza kwa kuzingatia vipengele 2-3 vya lugha ya kiubunifu. | Anazungumza kwa kuzingatia kipengele 1 cha lugha ya kiubunifu. |

MADA: KUSOMA

| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kusoma kwa ufahamu - Vifungu/ maigizo/ mashairi.** *(Ujumbe, umbo, wahusika matumizi ya msamiati mwafaka, kutoa muhtasari)* | Anasoma vifungu, maigizo na mashairi na kutambua ujumbe, umbo, wahusika, na matumizi mwafaka ya msamiati kwa utendeti. | Anasoma vifungu, maigizo na mashairi na kutambua ujumbe, umbo, wahusika na matumizi mwafaka ya msamiati. | Anasoma baadhi ya vifungu, maigizo na mashairi na kutambua ujumbe, umbo, wahusika na matumizi mwafaka ya msamiati. | Anasoma baadhi ya vifungu, maigizo na mashairi na kutambua kwa kiasi ujumbe, umbo, wahusika na matumizi mwafaka ya msamiati. |
| **Kuweza kusoma kwa kina.** *(Matumizi ya kamusi: mpangilio na maana za maneno na utumizi wa maneno)* | Anatumia kamusi kwa kuzingatia mpangilio, maana na utumizi wa maneno kwa urahisi. | Anatumia kamusi kwa kuzingatia mpangilio, maana na utumizi wa maneno. | Anatumia kamusi kwa kuzingatia mpangilio na maana ya maneno. | Anatumia kamusi kwa kuzingatia mpangilio maneno. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kusoma kwa ufasaha.** (*Matamshi bora, kiwango kifaacho cha sauti, kasi ifaayo, ishara zifaazo*) | Anasoma kwa kuzingatia vipengele 4 vya kusoma kwa ufasaha kikamilifu. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele 3 vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele 2 vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia kipengele 1 cha kusoma. |
| **Kuweza kusoma kwa mapana.** *(tahajia, sarufi, wahusika na ujumbe)* | Anasoma matini ya kujichagulia na kuzingatia vipengele 4 katika usomaji. | Anasoma matini ya kujichagulia na kuzingatia vipengele 3 katika usomaji. | Anasoma matini ya kujichagulia na kuzingatia vipengele 2 katika usomaji. | Anasoma matini ya kujichagulia na kuzingatia kipengele 1 katika usomaji. |
| **Kuweza kusoma kidijitali. (***Kufungua faili ya kidijitali, matumizi ya vifaa vya kidijitali, kusakura matini kwenye tovuti salama, kuchagua matini, kusoma matini, kutambua ujumbe na matumizi ya lugha.)* | Anasoma matini ya kidijitali akizingatia vipengele 6-7 ifaavyo. | Anasoma matini ya kidijitali akizingatia vipengele 4-5 ifaavyo. | Anasoma matini ya kidijitali akizingatia vipengele 2-3 ifaavyo. | Anasoma matini ya kidijitali akizingatia kipengele 1 ifaavyo. |

**MADA: KUANDIKA**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kuandika aina mbalimbali za insha** (*wasifu, masimulizi, maelezo na barua ya kirafiki)* kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: muundo, ujumbe, mtindo na kanuni zifaazo za uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele 4 vya uandishi ifaavyo. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele 3 vya uandishi ifaavyo. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele 2 vya uandishi ifaavyo. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia kipengele 1 cha uandishi ifaavyo. |

| Vigezo \ Viwango | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| **Kuweza kuandika kwa tarakilishi.** (*Sehemu za tarakilishi: kiibodi, kipanya, kiwambo, kitufe* na *faili).* | Anaweza kutambua sehemu 5 za kimsingi za tarakilishi za kupiga chapa. | Anaweza kutambua sehemu 4 za kimsingi za tarakilishi za kupiga chapa. | Anaweza kutambua sehemu 2-3 za kimsingi za tarakilishi za kupiga chapa. | Anaweza kutambua sehemu 5 za kimsingi za tarakilishi za kupiga chapa. |

**MADA: SARUFI**

| Vigezo \ Viwango | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kutambua na kutumia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili.** (*Vitenzi, viwakilishi, vielezi, viunganishi, vihusishi na vihisishi)* | Anatambua na kutumia aina 6 za maneno katika matini kwa kina. | Anatambua na kutumia aina 4-5 za maneno katika matini kwa kina. | Anatambua na kutumia aina 2-3 za maneno katika matini. | Anatambua na kutumia aina 1 ya neno katika matini kwa kina. |
| **Kuweza kutambua viambishi vya ngeli, nomino za ngeli na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo.** (A-WA, U-I, KI-VI, LI-YA na LI - LI) | Anatambua viambishi vya ngeli 5, nomino za ngeli na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo. | Anatambua viambishi vya ngeli 4, nomino za ngeli na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo. | Anatambua viambishi vya ngeli 2-3, nomino za ngeli na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo. | Anatambua viambishi vya ngeli 1, nomino za ngeli na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kutambua na kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali.** *(kauli ya kutenda, kutendea na kutendwa)* | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli 3 za mnyambuliko wa vitenzi. | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli 2 za mnyambuliko wa vitenzi. | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli 1 ya mnyambuliko wa vitenzi. | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli 1 ya mnyambuliko wa vitenzi kwa kutatizika. |
| **Kuweza kutambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika matini (***rafiki – adui, mgeni – mwenyeji, furaha – huzuni, uhuru-utumwa, mfalme- malkia, usiku – mchana, tajiri – maskini)* | Anatambua vinyume 6-7 vya maneno na kuvitumia katika matini. | Anatambua vinyume 4-5 vya maneno na kuvitumia katika matini. | Anatambua vinyume 2-3 vya maneno na kuvitumia katika matini. | Anatambua kinyume 1 cha neno na kukitumia katika matini. |
| **Kuweza kutambua na kutumia viambishi vya nyakati katika vitenzi.** (*Wakati uliopita, uliopo na ujao*) | Anatambua na kutumia viambishi vya nyakati 3 katika vitenzi kwa utendeti. | Anatambua na kutumia viambishi vya nyakati 3 katika vitenzi. | Anatambua na kutumia viambishi vya nyakati 2 katika vitenzi | Anatambua na kutumia viambishi vya wakati 1 katika vitenzi |
| **Kuweza kutambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha maneno ipasavyo.** (*Wakati uliopita, uliopo na ujao*) | Anatambua maneno 6-7 yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha maneno ipasavyo na kwa wepesi. | Anatambua maneno 4-5 yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha maneno ipasavyo. | Anatambua maneno 2-3 yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha maneno ipasavyo. | Anatambua neno 1 lililokanushwa, kiambishi cha ukanushaji na kukanusha neno. |

**Shughuli Jumuhishi ya Huduma ya Jamii ya Gredi 4-6**

Katika kiwango hiki, lengo la shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji ni kupata uwiano kati ya dhana zilizofunzwa katika masomo mbalimbali na maisha ya kila siku. Wanafunzi wenye changamoto za kuona wanafanya ulinganisho kati ya kile wamejifunza na maisha yao ya kila siku. Shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji imeshughulikiwa katika somo la *Social studies*. Utekelezaji wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji inahitaji ushirikiano ambapo mwalimu anashirikiana na walimu wa masomo mengine kuandaa na kutekeleza shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji. Ingawa shughuli hizi zinaelekezwa na mwalimu, mwanafunzi aliye na changamoto za kuona anatakiwa kupewa nafasi ya kutambua changamoto/tatizo na kuzua utatuzi wake. Usalama wa mwanafunzi unatakiwa kuzingatiwa katika utambuzi wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji. Hatua zifuatazo za shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji zinatakiwa kusambazwa katika mihula yote**.**

| **Hatua za utekelezaji wa shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji** |
|---|
| 1) **Maandalizi**<br>● Tambua umilisi wa kimsingi unaolengwa, maadili na stadi zinazokusudiwa katika matokeo maalum yanayotatarjiwa kwa mujibu wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji.<br>● Tambua nyenzo hitajika katika shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji (zinazopatikana katika mazingira)<br>● Kusambaza shughuli hizo katika muhula mzima (bainisha siku na wakati/muda wa shughuli hizo).<br>● Wasiliana na wanafunzi, wazazi/walezi, wasimamizi wa shule, walimu na washikadau wengine katika jamii ya shule.<br>● Tambua na kuandaa vifaa vya tathmini. |
| 2) **Utekelezaji wa Shughuli Jumuhishi ya Huduma ya Jamii.**<br>● Gawia wanafunzi majukumu.<br>● Hakikisha kila mwanafunzi anashriki kikamilifu katika shughuli husika.<br>● Tazama wanafunzi wanapotekeleza shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji na kurekodi matokeo ya utekelezaji wao.<br>● Tumia kifaa cha tathmini kinachofaa kutathmini mchakato mzima pamoja na matokeo yake (tathmini kazi ya mwanafunzi kuanzia mwanzo hadi mwisho).<br>● Tathmini umilisi wa kimsingi unaolengwa, maadili na stadi katika somo. |

**3) Tafakuri kuhusu Shughuli ya Huduma Jumuhishi ya kijamii.**

Chukua nafasi ya kujitathmini kuhusu shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji ukiwa na wanafunzi kwa kujadiliana nao kuhusu yafuatayo:

- Ni nini kilifanyika vizuri na kwa nini
- Ni nini hakikufanyika vizuri na kwa nini
- Ni nini kinaweza kufanywa tofauti
- Wamejifunza nini

Kutakuwa na shughuli moja jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji itakayotekezwa mara moja kwa mwaka. Masuala ya shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji yatatokana na masuala mtambuko pana katika masomo tofautitofati. Waalimu wanatakiwa kuangazia suala tofauti kila mwaka ili kuwapa wanafunzi fursa ya kushughulikia masuala mtambuko mbalimbali katika miktadha yao.

Shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji itashirikisha kila mmoja katika jamii ya shuleni (wanafunzi, wazazi/zalezi, wasimamizi wa shule na walimu). Wazazi/walezi ni washikadau muhimu katika maandalizi na utekelezaji wa shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji. Ingawa walimu wana jukumu muhimu katika maandalizi na ujumuishaji wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji, wanafunzi wanatakiwa kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima.
Shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji inampa mwanafunzi nafasi ya kukuza umilisi wa kimsingi na maadili mbalimbali. Mwalimu anatakiwa kubadilisha umilisi wa kimsingi na maadili yanayoangaziwa kila mwaka.

**Tathmini ya shughuli Jumuhishi ya Huduma ya Jamii.**

Tathmini ya Shughuli jumuishi ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji itaangazia vipengele vitatu ambavyo ni: stadi katika masomo mbalimbali yaliyoshirikishwa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji, umilisi wa kimsingi na maadili yanayodhihirishwa. Ni lazima tathmini izingatie mchakato mzima pamoja na matokeo ya shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji. Mwalimu atawatathmini wanafunzi wakiwa katika vikundi akitumia vifaa vya tathmini kama vile ratiba ya ukaguzi, orodha hakiki, viwango vya ukadiriaji au kifaa kingine kinachafaa.

## MAPENDEKEZO YA NYENZO ZA KUFUNDISHIA

| | | |
|---|---|---|
| Kapu maneno | Tarakilishi/vipakatalishi Vyenye teknolojia saidizi | Nakala ya shairi |
| Mti maneno | Kinasasauti | Kielelezo cha insha ya wasifu |
| Kadi za maneno/ orodha maneno,kadi za breli | Rununu yenye teknolojia saidizi | Kielelezo cha insha ya masimulizi |
| Picha za vitu mbalimbali/ maelezo ya picha | projekta | Kielelezo cha insha ya maelezo |
| Michoro/ maelezo ya michoro | Kamusi mbalimbali | Nyenzo halisi |
| Chati/chati nundu | Nakala ya barua ya kirafiki | Mgeni mwalikwa |
| Mabango | Sanamu | |

## MAPENDEKEZO YA MBINU ZA KUTATHMINI

- Kumakinikia jinsi mwanafunzi anavyotumia lugha katika mawasiliano
- Kutambua k.m. kwenye orodha au orodha maneno
- Kutunga sentensi k.m. kwa kutumia msamiati lengwa
- Kuambatanisha maneno lengwa
- Kujaza nafasi
- Kuandika tungo mbalimbali
- Kujibu maswali k.m. katika ufahamu
- Kutoa muhtasari wa ufahamu au matini yaliyosomwa
- Kujaza fumbo maneno

- Kazi mradi
- Kukariri na kuimba mashairi

**MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI**

- Kazi ya vikundi
- Vyama vya ushirika shuleni
- Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali ya mtambuko
- Ziara za nyanjani
- Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi